SportPesa
TZS. 642,668,240
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**MIAMALA** inayodaiwa kufanywa na Mbowe yawasilishwa korti kuu

UKURASA 3


Mwaka 1 wa Mwinyi Zanzibar...
siasa
HABARI BORA NA KAMILIFU
MIEZI SITA YA RAIS SAMIA
Undani wa ufanisi wake kuelekea kileleni miaka 60 Uhuru wa nchi
ACT-Wazalendo yaibuka na nguvu mpya
Kukoleza moto katiba mpya, tume huru

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Novemba 3, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII


ISSN 0856 • Na. 0580753

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.insta... ...ewspaper ...OW US


# Spika Ndugai awasha moto

**AHOJI** kuchelewa marekebisho sheria mafao, bima kwa wote, asema Bunge limechoka... *Endelea ukurasa 2*



Spika Job Ndugai

## Bodi, vigogo wa TANESCO kuhojiwa kukatika ovyo kwa umeme

UKURASA 3

UKURASA WA 4

### ASAKWA MADAI YA KUMNYONGA MKE HADI KUFA

POLISI mkoani Ruvuma inamsaka Exaveri Ngwenya (60) kwa tuhuma za kumuua mke wake, Vestina Elenziani (60), kwa kumnyonga shingo hadi kufa...

UKURASA WA 4

### MAFURIKO WANAFUNZI SHULE ZA AWALI

SERIKALI imeshauriwa kuendelea kuajiri walimu ili kukabiliana na tofauti ya uwiano kati yao na wanafunzi hasa shule za awali ambazo mwalimu mmoja anafundisha watoto 299.
Kiwango sahihi cha...

UKURASA WA 4

### BALOZI MAREKANI ATOA MAMILIONI MIRADI YA JAMII

UBALOZI wa Marekani nchini kupitia Mfuko wa Balozi wa kusaidia miradi ya maendeleo inayoendeshwa na wanajamii wenyewe umetoa ruzuku kwa miradi...



## Rais Samia ataja athari mabadiliko ya tabianchi kwa Tanzania

UKURASA 19

**MICHEZO** SIMBA, NAMUNGO LEO USHINDI TU KWA MKAPA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akijadiliana jambo na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Ndugai awasha moto Bungeni

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, jana aliwasha moto bungeni kutokana na kuchelewa kuwasilishwa bungeni kwa muswada wa mabadiliko ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma.

Hatua hiyo amesema inawafanya watumishi wa umma kutokujua hatima ya maisha yao baada ya kustaafu na kwamba wengi waliofikia umri wa kustaafu wanachanganyikiwa, kutokana na hali hiyo, amesema kama serikali imeshindwa, ipekele bungeni na Bunge litatunga sheria.

Ndugai alisema hayo jana bungeni baada ya Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Ester Bulaya, kuomba mwongozo kuhusu serikali kuchelewa kuleta muswada wa marekebisho ya sheria hiyo.

Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma No. 2 ilipitishwa na Bunge Januari 31, 2018 kwa kuunganisha mifuko ya PPF, PSPF, LAPF na GEPF na kuunda PSSSF ambayo ina wajibu wa kuhudumia watumishi wa umma.

Sheria mpya ndiyo ilileta kikokotoo kipya ambacho kilitaka mstaafu kulipwa malipo ya mkupuo ya asilimia 25, huku asilimia 75 akilipwa kidogo kidogo, utekelezaji ambao kabla ulikuwa uko NSSF, huku mifuko mingine ikiwamo PSPF wakilipa asilimia 50.

"Tukumbushane jambo moja tu, kwa mtu aliyefanya kazi serikalini kwa miaka mingi kwa uaminifu na uadilifu anapofikia muda wa kustaafu halafu haelewi hatima yake. Si jambo jepesi kwa sababu unaondoka kwenye maisha uliyozoea unaingia kwenye maisha mengine. Watu wengi wanaogopa kustaafu. Kustaafu ni usiku wa giza," alisema.

"Kwa hiyo mtu anataka kujua anakwenda kwenye maisha gani. Hicho ndicho tunakiongelea hapa. Kwa hiyo tuwaombe wenzetu kulipa kipaumbele suala hili kwa sababu wadau wote hao wapo. Hakuna aliye nje ya nchi. Mkutane kwa haraka mmalize mambo

"Tena vyama vya wafanyakazi ndiyo wadau wenyewe wa jambo hili, mmalize haraka na muache mambo ya posho kuwa na vikao vingi, mlimalize ili na sisi Bunge tutende haki. Uhakika wa wastaafu wetu lazima ufahamike, watu wanachanganyikiwa. "Tunaomba serikali mmalize haraka mchakato huo. Kama unawasumbua tuleteeni bungeni sisi tutatunga," alisema.

**KAULI YA BULAYA**

Akiomba mwongozo, Bulaya alisema ratiba ya mkutano wa tano wa Bunge haionyeshi sehemu yoyote kuletwa kwa muswada wa marekebisho wa Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kama ilivyoahidiwa na serikali wakati wa mkutano wa nne wa Bunge.

"Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. Nimeangalia ratiba ya bunge hakuna kabisa kuletwa kwa muswada wa marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma.

"Nakumbuka Muswada wa Sheria ya marekebisho ya Jeshi la Zimamoto ilitungwa muda huohuo, lakini ikaletwa bungeni na kufanyiwa marekebisho. Naomba mwongozo wako serikali iseme kwa nini hawajaleta? Lini wataleta? Kwa sababu tunataka maslahi ya Watanzania yafanyiwe kazi," alisema.

**KAULI YA SERIKALI**

Akilitolea ufafanuzi suala hilo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi na Ajira), Jenister Mhagama, alisema: "Maelekezo yaliyotolewa na Hayati Rais John Magufuli suala hili lilipelekwa kwa serikali na wadau wa sekta ya hifadhi ya jamii ambao ni serikali, wadau na waajiri".

Mhagama ambaye ni Mnadhimu Mkuu wa Serikali bungeni alisema Hayati Rais Magufuli kupitia serikali alitoa kipindi cha mpito ambacho kinaisha mwaka 2022/23 muda ambao bado uko mbele.

Alisema jambo hilo lilikuwa na maelekezo kadhaa moja ikiwa ni kuendelea na utaratibu uliokuwa unaendelea wa kusimamia sekta ya hifadhi ya jamii.

Mhagama alisema pili ilikuwa ni lazima kuhakikisha kabla ya kutengeneza mfumo mpya wa hifadhi ya jamii lazima kufanyike utathmini wa kutosha wa hali ya sekta, mazingira yalivyo, kisha kuja na mfumo ambao utakuwa endelevu kwa ustawi wa wafanyakazi, lakini vile kwa ustawi wa sekta yenyewe.

"Ni kweli serikali tulisema tunakusudia kuleta muswada huo, lakini sheria yoyote inayoletwa bungeni ni lazima ifanyiwe kazi kwa viwango vya kutosha, uwe shirikishi na inapoletwa bungeni iwe endelevu ambayo itaakisi muktadha wa sekta inayohusiana na sheria hiyo.

"Kwa sasa utathmini wa mifuko umeshafanyika, baada ya hapo kazi inayotakiwa kufanyika kabla ya sheria hiyo kukamilika ni wadau wote, vyama vya wafanyakazi, serikali na vyama vya waajili kuipitia ripoti hiyo na kutoa maoni ya pamoja na baada ya hapo sasa tukubaliane marekebisho yanayotakiwa kufanyika yawe ni marekebisho gani ambayo yanakwenda kujibu hoja ambazo zipo mezani katika sekta ya hifadhi ya jamii," alisema.

## Bima kwa wote yawa kaa la moto

**Gwamaka Alipipi, DODOMA**

BUNGE limehoji sababu za kuchelewa kwa uwasilishwaji wa Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote bungeni, kuitaka serikali kuharakisha mchakato wake.

Limesema bima ya afya kwa wote inagusa Watanzania wengi hususani walio masikini, hivyo ni muda mwafaka kuletwa muswada bungeni ili itungiwe sheria, kwamba suala hilo limekwama kwa muda wa miaka mitano hadi sasa.

Kwa mujibu wa serikali, Sh. bilioni 149 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa bima ya afya kwa wote.

Akizungumza bungeni jana, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alieleza kushangazwa na mchakato wa kukamilisha muswada huo ambao alisema unachukua muda mrefu wakati suala hilo linagusa asilimia kubwa ya Watanzania.

"Unajua kuna jambo unalitenda kwa kutenda au kutokutenda. Sasa hili la bima ya afya kwa wote tulishindwa miaka mitano iliyopita. Tulikumbusha kila Bunge, mabunge yote 19. Sasa tunahesabu Bunge la tano hili, tunazidi kwenda lakini mchakato haukamiliki," alisema.

"Hivi huku serikalini kuna nini kisichoisha ambacho ni michakato isiyoisha, mnajadili nini? Bima ya afya ndicho kipaumbele kwa Watanzania mwaka huu, sasa sijui mnakwama wapi?" alihoji.

Ndugai alisema mabunge ya kutunga sheria yako machache sana na kwamba linaloendelea sasa ni la mipango, litakalofuata ni la bajeti, kwa hiyo mabunge ya kutunga sheria yapo machache.

"Tusipoyatumia mabunge ya kutunga sheria ambazo ni muhimu itakuwa kila siku tunakuja na mabadiliko ya sheria mbalimbali lakini zile ambazo ni muhimu tunazodaiwa na Watanzania ndizo zinacheleweshwa," alisema.

Ndugai alisema kwa mujibu wa ratiba za Bunge, sheria hiyo inapaswa kukamilika mapema Novemba, mwakani, vinginevyo itakwenda hadi mwaka 2023.

Spika Ndugai alisema agenda zinginezo ni 'by the way' lakini bima ya afya ndicho kipaumble namba moja kwa Watanzania. Alisema Bunge la 11 wakati linamalizika na linakuja Bunge la 12 kazi mojawapo iliyoshindikana kwenye ilikuwa ni kutunga Seria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Alisema hivyo matarajio ya Watanzania ni Bunge la 12 lifanikishe kutungwa kwa sheria hiyo.

Aidha, Spika Ndugai aliitaka Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kulikazania suala hilo kwa kuhakikisha linakamilika na muswada unaletwa bungeni ili itungwe sheria. Alisema kamati ya Bunge ikikaa kimya pasipo kuweka msukumo kwa wahusika mchakato huo utazidi kukwama.



Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Mkoa wa Dar es Salaam, Hemed Mkali, akizungumza katika kikao cha Kamati ya Huduma ya Afya ya Msingi, katika ukumbi wa Karimjee, mkoani humo, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Miamala inayodaiwa kufanywa na Mbowe yawasilishwa korti kuu

**Na Kulwa Mzee**

MWANASHERIA wa Kampuni ya MIC Tanzania Limited, maarufu Tigo, Fredy Kapara, amedai namba aliyopewa kuchunguza ilikuwa 0719933386 ya Freeman Mbowe, ilituma Sh. 500,000 kwenda kwa Luteni Dennis Urio aliyekuwa anatumia namba 0787555200 iliyoonekana kwenye usajili.

Kapara pia amedai hafahamu kama Freeman Elikaeli Mbowe ni kiongozi wa chama kikuu cha upinzani na kwamba kuna Freeman Mbowe wengi.

Shahidi huyo wa tano wa upande wa mashtaka alidai hayo alipokuwa akitoa ushahidi Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mbele ya Jaji Joackim Tiganga jana.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Nassoro Katuga, shahidi huyo alidai kuwa Julai 2021, alipokea barua kutoka kwa Kamishna wa Upelelezi wa Kisayansi akitaka taarifa za mteja mwenye namba 0719933386, akiomba miamala kuanzia Juni Mosi, mwaka 2020 hadi Julai 31, mwaka 2020.

Alidai alivyoingiza namba hiyo katika mfumo, alipata taarifa hizo na akazichapisha na kuziwasilisha zilikohitajika.

Aliomba kutoa kama kielelezo barua aliyoombwa kuchunguza namba, barua aliyoandika baada ya uchunguzi, taarifa za miamala ya fedha na taarifa za usajili.

Upande wa Jamhuri haukuwa na pingamizi kwa vielelezo hivyo kupokewa, Mahakama ilipokea na kuvipa P6, P7, P8 na P9.

Akisoma vielelezo hivyo, shahidi huyo alidai namba 0719933386 ilituma fedha Sh. 500,000 akiwa maeneo ya Mikocheni wilayani Kinondoni kwenda kwenye namba 0787555200 ambayo hakutaja jina kwa madai taarifa za namba hiyo zinapatikana Aitel.

Namba hiyo iliyotumiwa fedha katika kuangalia kwenye usajili inasoma jina la Dennis Urio ambaye anatajwa katika kesi hiyo ya ugaidi kuwa miongoni mwa shahidi.

Luteni mstaafu Dennis Urio katika maelezo ya ushahidi yaliyopo mahakamani, anadaiwa alipewa kazi na Mbowe ya kumtafutia makomandoo waliofukuzwa kazi jeshi au waliostaafu ili afanye nao kazi.

Alidai kuwa namba 0719933386 alipochunguza usajili, alibaini ilisajiliwa awali mwaka 2016 na ikasajiliwa kwa mara ya pili kwa alama ya vidole Julai 16, 2019.

Shahidi huyo alidai kuwa baada ya kukamilisha uchunguzi, aliitwa Julai 8, mwaka huu Kituo cha Polisi cha Kati kwa ajili ya kutoa maelezo, alikwenda na kutoa maelezo.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Jeremiah Mtobesya, shahidi alidai wakati anatoa ushahidi hakusema kama kuna wakati wataalamu wa mitandao wanajaribu ama kuingia kwenye simu kuchukua ama kuharibu taarifa ama mfumo.

Alidai hakusema kama wakati anachunguza, alizuia uwezekano wa wataalamu hao kuingilia ama kuvuruga taarifa.

Akihojiwa na Wakili John Mallya, alidai hajui jina la aliyemsajili Mbowe kwa alama za vidole kwa sababu katika taarifa iliyotoka, hakuona jina.

Alidai barua ilifika kwake ikitaka achunguze namba hiyo ya Tigo na haikueleza kosa husika na aliongeza kuwa si lazima kuwapo.

Shahidi huyo akihojiwa na Wakili Peter Kibata, alidai hafahamu kama Freeman Elikaeli Mbowe ni kiongozi wa chama kikuu cha upinzani na kwamba Freeman Mbowe wako wengi.

Alidai alipoombwa taarifa za mteja, hakumtaarifu Mbowe kwamba taarifa zake zinahitajika na hakuchukua hatua yoyoye ya kuomba mwongozo wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Kapara alikiri kwamba barua aliyoandikiwa akiombwa kuifanyia uchunguzi namba 0719933386, ilikuwa ya jalada la kesi ya mwaka 2020 lakini majibu yake baada ya uchunguzi alinukuu jalada la kesi ya mwaka 2021.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Halfani Bwire ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei Mosi na Agosti 5, 2020 katika mikoa ya Morogoro, Moshi, Arusha, Dar es Salaam, Mbeya na Mwanza.

# Bodi, vigogo wa TANESCO kikaangoni kukatika umeme

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

TATIZO la kukatika kwa umeme ovyo nchini limemsukuma Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuiagiza Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuiita haraka Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), pamoja na uongozi wa Wizara ya Nishati ili kuhakikisha kero hiyo inamalizika.

Amesema kilio cha kukatika kwa umeme mara kwa mara nchini kimekuwa sugu, wananchi wengi wanalalamika na kushindwa kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Alitoa agizo hilo jana bungeni baada ya kuwapo kwa maswali mengi kutoka kwa wabunge yakielekezwa kwa Waziri wa Nishati ya kukatika kwa umeme katika maeneo yao.

"Naona maswali mengi kutoka kwa wabunge kuhusiana na umeme. Hii ina maana kukatika kwa umeme mara kwa mara ni tatizo kubwa," alisema.

"...Kaeni na wizara (Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini), iiteni bodi ijue undani wa tatizo hili. Tatizo linazidi kuwa kubwa. Mfahamu mipango ya (kutoka wizarani) ikiwa inaridhisha," alisema.

Awali, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, aliwaambia wabunge mabadiliko ya haraka yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu TANESCO hayakwepeki katika kuboresha utendaji wake unaojumuisha ukusanyaji wa mapato.

Byabato alisema mabadiliko yaliyofanywa na serikali katika shirika hilo yatasaidia kumaliza kukatika kwa umeme.

**WALICHOSEMA WABUNGE**

Mbunge wa Manyoni-Magharibi, Yahaya Masare (CCM), alifungua mjadala wa kero za umeme akieleza kwamba baadhi ya wateja wa TANESCO jimboni kwake wameondolewa kutoka watumiaji wa huduma ya chini ya umeme kwenda kwa watumiaji wa kati.

Alisema mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijijini (REA) awamu ya tatu hajaripoti kazini.

Wabunge wengine waliolalamikia kukatika umeme ni pamoja na Mbunge wa Kilombero, Abubakar Asenga (CCM), Mbunge wa Jang'ombe, Ali Hassan King (CCM) na Mbunge wa Viti Maalum, Taska Restituta Mbogo.

# Bei ya dizeli yashuka

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

BEI ya mafuta ya dizeli imeshuka kwa Sh. 18 katika Bandari ya Dar es Salam kutoka Sh. 2,261 Oktoba na kufikia Sh. 2,043 mwezi huu huku bei ya petroli ikibaki ile ile.

Akitangaza kushuka kwa bei ya mafuta hayo jana jijini Arusha, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mhandisi Godfrey Chibulunje, alisema mafuta hayo yameshuka kutokana na jitihada za serikali kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo kwa bei nafuu licha ya soko la dunia kupanda.

Alisema bei hiyo ya mafuta ya dizeli itaanza kutumika leo na kusisitiza bei ya petroli kuwa hivyo hivyo kama awali ya Sh.2 439 kwa lita moja.

Alisema bei ya mafuta ya taa katika Bandari ya Dar es Salaam itaendelea kuwa Sh. 2,188 na katika Bandari ya Tanga bei ya mafuta ya petroli ilikuwa ni Sh.2478 kwa lita moja huku dizeli ilikuwa inauzwa Sh.2245 kwa lita moja.

Alisema katika Bandari ya Mtwara bei ya mafuta itabaki kama ilivyo, petroli itakuwa ni Sh. 2,455 na dizeli Sh. 2,279 huku bei ya mafuta ya taa ikiwa ni Sh. 2,260.


**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

***Kwa Idhini tuliyopewa na BANK OF AFRICA*** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba pamoja na gharama za dalali. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo wake kwa MNADA WA HADHARA.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | WANTANSHI LOUNGE | Nyumba ya makazi yenye Hati na.23659 Kiwanja na.1318 Ofisi ya ardhi na.39847 iliyopo Msasani Peninsular | 20/11/2021 |

**MASHART YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) Ltd**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor**
**P.O. BOX 1088**
**Dar Es Salaam.**
**Mob: + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Bank of Africa**
**Head Office,**
**NDC Development House, Ohio street/kivukoni**
**P.O. BOX 3054,**
**Dar Es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255-22-2110104/2111290**
**Fax: +255-22-2113740**

116549602

# Asakwa na polisi madai ya kumnyonga mke hadi kufa

**Na Gideon Mwakanosa, SONGEA**

POLISI mkoani Ruvuma inamsaka Exaveri Ngwenya (60) kwa tuhuma za kumuua mke wake, Vestina Elenziani (60), kwa kumnyonga shingo hadi kufa akiwa jikoni nyumbani kwake.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Amini Mahamba, alisema tukio hilo limetokea Oktoba 30, majira ya sa 3:00 usiku, mtaa wa Ruvuma juu.

Alisema inadaiwa siku hiyo ya tukio kulikuwa na ugomvi kati ya wawili hao baada ya mume kutoka matembezini akiwa amelewa na ugomvi huo uliendelea hadi majirani waliposikia kelele za mayowe zilizosababisha wafike kwenye eneo la tukio.

Alisema wakati majirani wanafika eneo la tukio, Ngwenya alikuwa ameshamuua mke wake kwa kumnyonga na taarifa kufikishwa kituo kikuu cha Songea.

Alifafanua kuwa inadaiwa kuwa Ngwenya baada ya kumshushia kipigo mke wake na kumyonga alikimbia na kutokomea kusikojulikana na polisi inaendelea kumsaka mtuhumiwa huyo huku chanzo cha mauaji hayo kikidaiwa kuwa ni ulevi.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo (katikati), akizungumza na Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omari Kumbilamoto (kushoto), wakati wa kikao cha tathmini ya utoaji wa chanjo ya Uviko-19, jijini humo, jana. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mafuriko wanafunzi shule za awali

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imeshauriwa kuendelea kuajiri walimu ili kukabiliana na tofauti ya uwiano kati yao na wanafunzi hasa shule za awali ambazo mwalimu mmoja anafundisha watoto 299.

Kiwango sahihi cha uwiano kinachotakiwa ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 25.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi kwenye sekta ya elimu, ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la HakiElimu, Dk. John Kallaghe, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye mkutano wa mwaka wa tathmini ya maendeleo ya sekta ya elimu.

Alisema kuna upungufu mkubwa wa walimu licha ya kuwapo wa jitihada mbalimbali za serikali kuajiri.

"Mfano uwiano kati ya wanafunzi na walimu kwenye elimu ya awali ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 299, ambapo kwa viwango vyetu inatakiwa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 25, ili kuwaandaa watoto vizuri kwenye elimu ya awali ni kuhakikisha walimu wapo," alisema.

Alisema udahili umeongezeka kwa kiasi kikubwa kwa mfano watoto wote ambao wapo elimu ya awali hadi sekondari wameongezeka kutoka milioni 14.7 kwa mwaka 2019/20 hadi milioni 15.2 kwa mwaka 2020/21. Alibainisha kuwa ongezeko hilo limetokana na jitihada mbalimbali ambazo zinafanywa ikiwamo utoaji wa elimumsingi bila malipo.

Katika hatua nyingine, Dk. Kallaghe alisema Ripoti ya Elimumsingi ya mwaka 2020, inaonesha wanafunzi wa kike 119,591 wamekumbwa na mdondoko kwenye shule za msingi na sekondari nchini kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo mimba. Alisema takwimu zinaonesha kuna mdondoko mkubwa kwa watoto wa kike ikilinganishwa na wa kiume na uwiano unaonesha kwa sekondari ni mtoto wa kiume mmoja kwa wa kike wawili (1:2).

"Kwa ripoti ya BEST 2020, wasichana 71,151 walikumbwa na mdondoko kwa shule za msingi na 48,440 kwa sekondari kutokana na sababu mbalimbali hasa mimba bado ni tatizo kubwa ambapo inaonesha kwa mwaka huo kulikuwa na wanafunzi 1,135 wa shule za msingi na sekondari 5,398 walioacha shule kwasababu ya mimba," alisema.

Aidha, alisema katika miaka minne iliyopita (2016-2019) watoto 21,494 waliacha shule kwasababu ya mimba.

Mwenyekiti huyo alisema licha ya kuwepo kwa jitihada za kuhakikisha vikwazo vinavyomzunguka mtoto wa kike vinapungua lakini serikali ni vyema ikafungua mjadala kuhusu mwongozo unaoruhusu watoto kurudi shule moja kwa moja.

Hata hivyo alisema bajeti ya sekta ya elimu licha ya kuongezeka bado ipo chini katika viwango vya uwekezaji kwenye sekta hiyo kimataifa.

Akifungua mkutano huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, alisema serikali inaendelea na jitihada za kuwarudisha shule wanafunzi walioacha katika ngazi ya sekondari na msingi.

"Kwa mwaka 2020/21 wanafunzi 3,668 wamerudi na kufanya mtihani wa darasa la saba na kujiunga na Kidato cha Kwanza (Wavulana 2353, Wasichana ni 1315). Pia tuliwarudisha shuleni kwa ngazi ya kidato cha tano jumla ya wanafunzi 288 (Wasichana ni 149, Wavulana ni 139) waliokuwa wameacha shule katika ngazi ya sekondari. Juhudi zetu hazitaishia hapo tutaziendeleza ili tuwarudishe wengi zaidi shuleni," alisema.

Kadhalika, Dk. Akwilapo aliwataka wadau hao kushiriki ipasavyo katika mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya elimu na kutoa maoni yao kwa uwazi ili kuendana na uhitaji wa sasa kwa maendeleo ya taifa.

## Balozi Marekani atoa mamilioni miradi ya jamii

**Na Mwandishi Wetu**

UBALOZI wa Marekani nchini kupitia Mfuko wa Balozi wa kusaidia miradi ya maendeleo inayoendeshwa na wanajamii wenyewe umetoa ruzuku kwa miradi sita ya kijamii yenye thamani ya Dola za Marekani 52,540 (sawa na Sh. milioni 121).

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Ubalozi huo ilisema, Balozi mdogo wa Marekani, Robert Raines, jana alitia saini makubaliano ya kutoa ruzuku hiyo ambayo husaidia wanajamii kujiendeleza tangu mwaka 1965, kwa miradi midogo midogo ya maendeleo ya jamii inayoendeshwa na jamii zenyewe nchini.

"Mfuko wa Balozi wa kusaidia miradi ya kijamii, ni programu muhimu inayoiwezesha Marekani kushirikiana moja kwa moja na vikundi vya kijamii vinavyofanyakazi kwa bidii kuleta maendeleo na mabadiliko chanya kwenye jamii zao.

"Naamini mabadiliko ya kweli na ya kudumu hutokea pale watu katika ngazi ya chini kabisa wanaposhirikiana kuleta mabadiliko chanya katika jamii zao. Mfuko huu ulianzishwa ili kuvisaidia vikundi vilivyoonyesha dhamira ya dhati ya kujiletea maendeleo, kwa miaka 50 mfuko umesaidia miradi midogo midogo kila mkoa," alisema.

Alivitaja vikundi vilivyopata ruzuku kuwa ni asasi ya Agro-Livestock and Welfare Advancement Rural Environment (AWARE), walipata Dola 9,692 (sawa na Sh. milioni 22.3), za kutekeleza mradi wa kujenga mfumo wa kuvuna maji ya mvua katika zahanati nne Wilaya ya Kalambo, mkoani Rukwa.

"Mradi huu utatatua tatizo la upatikanaji maji kwa jamii, hususan kwa vijana, wanawake, watu wenye ulemavu na watu wanaoishi na VVU. Kupitia mradi huu, matangi manne ya kuvuna maji ya mvua yatajengwa katika zahanati za Msanzi, Mkali, Katazi na Kasanga, kila tangi likiwa na uwezo wa kuchukua maji lita 20,000 yatakayokuwa yakikusanywa kutoka katika mapaa ya zahanati hizo," alisema.

Wengine ni asasi ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), mradi wa Bega kwa Bega Dola 10,634.27 (sawa na Sh. mil. 24.5) unaotekelezwa kwa ushirikiano na Asasi ya Kimarekani ya Saint Paul Partners, ambayo ina uzoefu wa zaidi ya miaka 19 katika utekelezaji wa miradi ya maji mkoani Iringa.

"Lengo la mradi huu ni kukipatia kijiji cha Magome, mkoani Iringa, majisafi na salama. Mradi huu unalenga kupeleka maji katika maeneo matatu yaliyoainishwa na wanakijiji wenyewe shule ya msingi, zahanati na eneo la soko na KKKT kupitia mfumo wa usambazaji maji wa mteremko," alisema.

# TANGAZO

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## IMEDURIWA - OMBI LA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA UCHAPISHAJI TAARIFA PAMOJA NA BIDHAA ZENYE CHAPA KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI.
## KUMBUKUMBU. 0010007126

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi na kampuni zenye weledi na uzoefu katika Nyanja ya uchapishaji wa nyaraka za mawasiliano katika mifumo mbalimbali pamoja na kutoa huduma ya bidhaa zenye chapa (Large Scale Printing and Products Branding) katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

KAMPUNI inahitaji huduma za kampuni ya mawasiliano kutoa usaidizi katika moja au huduma mbalimbali tajwa kulingana na mahitaji:

- Huduma ya uchapishaji taarifa za mawasiliano katika mifumo mbalimbali.
- Kutoa huduma ya bidhaa zenye chapa ikiwa ni pamoja na mbao za matangazo na masanduku ya maoni yenye chapa.

**VIGEZO MUHHIMU**

Makampuni au mashirika yatakayoonesha nia, yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa uzoefu wa utendaji kazi bora pamoja na sampuli za kutekeleza kazi za usaidizi katika mawanda ya mawasiliano ya nia husika, kampuni au Taasisi inaweza kuonyesha nia kwa zabuni moja au zaidi kati ya zilizoorodheshwa hapo juu. Katika hatua hii, sampuli zote za kazi za mawasiliano zinatakiwa kuwasilishwa kupitia uzi wa taarifa (link) ambao hautarajii kuisha muda wake.
- Uthibitisho wa uwezo mfano kuwa na vifaa, miundo mbinu pamoja na muundo wa timu ya watendaji.
- Uthibitisho wa kufanya kazi katika miradi mikubwa yenye uhitaji mkubwa wa usaidizi wa mawasiliano.
- Uthibitisho wa uzoefu na/au uwezo wa kusambaza na kubandika taarifa za mawasiliano katika ukanda wa kati katika mikoa ya Kagera, Geita, Tabora, Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga ikihitajika.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2020.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutoa usaidizi husika.
- Uzingatiaji wa Kanuni za Maudhui ya Wazawa za mwaka 2012 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Wazawa (Nafasi za Ajira na Huduma kwa Watanzania).
- Usajili stahiki kutoka kwa mamlaka za nchi zinazohusika kwa ajili ya kutoa huduma stahiki inapobidi.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha Mwaka wa Karibuni cha Malipo ya Kodi.

Mashirika yenye nia ya kuleta maombi na ambayo yana uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **11 Novemba 2021. Kichwa cha Baruapepe: 0010007126.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na mashirika yatakayoonesha nia ili kutengeneza orodha ya Mashirika ya awali yenye vigezo vinavyotakiwa. Mashirika yatakayokidhi vigezo tu ndiyo yatapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

2165505

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## LIMERUDIWA - OMBI LA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA USAIDIZI KATIKA KITENGO CHA MAWASILIANO KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI.
## KUMBUKUMBU: 0010007127

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi na kampuni zenye weledi na uzoefu katika Nyanja ya mawasiliano kuonesha nia ya kutoa huduma zinazohusiana na mawasiliano kwa Umma katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

KAMPUNI inahitaji huduma za kampuni ya mawasiliano kutoa usaidizi katika moja au huduma mbalimbali tajwa kulingana na mahitaji:

- Sanaa ya kusanifu michoro, picha, miundo na alama kwa kutumia technolojia ya komputa (Graphics designing)
- Sanaa ya kusanifu miundo, picha na alama zenye mwendo, michoro yenye mwendo mfumo wa 2D &3D pamoja na michoro ya vielelezo kwa kutumia teknolojia ya komputa.
- Sanaa za jukwaani haswa katika maeneo ya mkuza wa bomba: Kagera, Geita,Tabora, Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara and Tanga.
- Huduma ya Kurekodi video zenye viwango vya juu pamoja na kuzihariri.
- Huduma za upigaji picha pamoja na uhariri wa picha.
- Huduma za kurekodi sauti ikiwemo kuzihariri.
- Tafsiri kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili hasa katika mfumo wa maandishi.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au mashirika yatakayoonesha nia, yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa uzoefu wa utendaji kazi bora pamoja na sampuli za kutekeleza kazi za usaidizi katika mawanda ya mawasiliano ya nia husika, kampuni au Taasisi inaweza kuonyesha nia kwa zabuni moja au zaidi kati ya zilizoorodheshwa hapo juu. Katika hatua hii, sampuli zote za kazi za mawasiliano zinatakiwa kuwasilishwa kupitia uzi wa taarifa (link) ambao hautarajii kuisha muda wake.
- Uthibitisho wa uwezo mfano kuwa na vifaa, miundo mbinu pamoja na muundo wa timu ya watendaji.
- Uthibitisho wa kufanya kazi katika miradi mikubwa yenye uhitaji mkubwa wa usaidizi wa mawasiliano.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kufanya kazi katika ngazi za chini katika ukanda wa kati katika mikoa ya Kagera, Geita, Tabora, Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga Sanaa za majukwaani utapewa kipaumbele.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2020.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutoa usaidizi husika.
- Uzingatiaji wa Kanuni za Maudhui ya Wazawa za mwaka 2012 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Wazawa (Nafasi za Ajira na Huduma kwa Watanzania).
- Usajili stahiki kutoka kwa mamlaka za nchi zinazohusika kwa ajili ya kutoa huduma stahiki inapobidi.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha Mwaka wa Karibuni cha Malipo ya Kodi.

Mashirika yenye nia ya kuleta maombi na ambayo yana uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **11 Novemba 2021. Kichwa cha Baruapepe ni 0010007127.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na mashirika yatakayoonesha nia ili kutengeneza orodha ya Mashirika ya awali yenye vigezo vinavyotakiwa. Mashirika yatakayokidhi vigezo tu ndiyo yatapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

2165505

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Msako vituo bubu vya mafuta uwe endelevu

**JUZI** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilitangaza kuanza msako wa kubaini wafanyabiashara wanaouza mafuta ya taa, dizeli na petroli bila leseni.

Lengo la msako huo ni kudhibiti matukio ya moto yanayoweza kutokea maeneo mbalimbali, ambayo baadhi yameshuhudiwa kuangamiza mali na maisha ya watu.

Uuzaji holela wa mafuta umekuwa tatizo sugu na sasa yanauzwa kama zinavyouzwa karanga au pipi kando kando ya barabara kuu.

Watu wanaouza mafuta hayo hawazingatii viwango vinavyotakiwa kuhifadhi mafuta hayo na badala yake huwekwa kwenye chupa za maji zilizotumika na kuwekwa kwenye jua.

Biashara hii imeshamiri hasa maeneo ya kando ya mji na wateja wakubwa ni waendesha bodaboda na bajaji ambao hununua rejareja kwa wafanyabiashara hao.

Kinachohatarisha zaidi ni mafuta hayo kuhifadhiwa ndani ya nyumba za kuishi watu bila kuchukua tahadhari ya moto. Vidumu hivyo vinawekwa sehemu ambazo moto unapotokea sio rahisi kuudhibiti na pia kuleta madhara kwa watu wengine wanaoishi jirani na nyumba zinazohifadhi mafuta hayo.

Akizungumza na vyombo vya habari juzi, Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, George Mhina, anasema kanda hiyo inaoongoza kwa matukio ya nyumba kuwaka moto unaosababishwa na uhifadhi wa mafuta ya petroli na dizeli kwenye makazi ya watu.

Anasema kuuza nishati hiyo bila utaratibu ni kinyume cha maelekezo ya mamlaka hiyo na kuwataka watu wanaofanya biashara hiyo wajisalimishe wenyewe kabla ya msoko huo haujaanza.

Mafuta ni kimiminika hatari ambacho hukifadhiwa kwenye matangi yanayochimbiwa ardhini, lakini wafanyabiashara wadogo wanauza mafuta kwenye chupa za maji ya kunywa kwa kuziweka nje juani hali ambayo inaweza kusababisha mlipuko na kuyafanya yakose ubora yanapotumiwa kwenye vyombo vya moto.

Ewura inatoa leseni kwa wafanyabiashara wanaomiliki vituo vya mafuta waliokidhi vigezo vya kisheria. Kwa wale wanaouza kwenye mapipa, madumu na chupa hawatakiwi kwa mujibu wa sheria.

Mamlaka hiyo imeweka utaratibu unaowataka wamiliki wa vituo vya mafuta vilivyopo mijini kujenga vituo vingine hususani vijijini ili kudhibiti wimbi la wauzaji wa mafuta wasio na leseni.

Pia inafafanua kuwa uwekaji wa vinasaba katika mafuta ya taa, petroli na dizeli kabla ya kuingia sokoni umesaidia kupunguza uchakataji wa nishati hiyo kwa asilimia 80 na kupunguza malalamiko yaliyokuwa yanawasilishwa EWURA kuwa mafuta ni machafu.

Ni imani yetu kuwa msako huo unaotarajiwa kuanza utamaliza kama sio kupunguza tatizo la uchakachuaji mafuta.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Wapigakura wanachoka ahadi zisizotekelezeka



Na Sabato Kasika

**KILA** unapofanyika uchaguzi uwe wa urais, udiwani, ubunge hata umeya kuna ahadi kemkem zinazotolewa na wagombea kutoka vyama mbalimbali vya siasa kwenda kwa wapigakura kwa lengo la kuwashawishi na kuwavuta wamkubali.

Miongoni mwa ahadi hizo ambazo hutolewa na wanasiasa hao ujenzi au uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwamo ya barabara, madaraja, skimu za umwagiliaji na zahanati, lakini baadhi hazitekelezwi kulingana na jinsi walivyoahidi.

Inawezekana wapigakura wengi hushawishika kwa ahadi hizo za wakati wa kampeni bila kujua zinatekelezwa vipi, au ni fedha zipi zinazotumika kutekeleza ahadi hizo, badala yake hushangilia tu wanapoahidiwa.

Kutoelewa jinsi ya utekelezaji wa ahadi, kunaweza kuwafanya wagombea ubunge kupata kura kirahisi, kwa kuwa wanajua kwamba hata ikiwa ni ahadi hewa, wananchi hawana mwamko wa kuhoji.

Hivyo ingekuwa ni vyema wagombea wakawa wazi kuhusu jinsi ya kutekeleza ahadi wanazotoa wakati wa kampeni, kwamba watatumia fedha zipi kwa ajili ya kutekeleza ahadi hizo kuliko kuwaacha wananchi hewani.

Kwa wale wanaofuatilia siasa za Tanzania watakubaliana nami kwamba baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakitoa ahadi kwa wananchi ambazo matokeo yake huwa hawazitekelezi.

Mwanasiasa anaweza kuwa kwenye eneo ambalo lina ubovu wa barabara na kuahidi kwamba wananchi wakimchagua, atamaliza kero hiyo mara moja, hali ambayo huwafanya wamwamini, lakini badala yake ahadi hiyo haitekelezwi.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, wapo baadhi ya wagombea ubunge jijini Dar es Salaam waliotoa ahadi za kuboresha miundombinu ya barabara kwenye majimbo waliowania kwa kipindi kifupi.

Hata hivyo, unakaribia mwaka mmoja tangu kufanyika kwa uchaguzi, wengine hawajatekeleza ahadi hizo, waliahidi kuzimaliza ndani ya kipindi kifupi mara tu baada ya kuchaguliwa. Zipo barabara nyingi ambazo wanasiasa waliahidi kuziboresha, ikiwamo za majimbo ya wilaya ya Ubungo jijini Dar es Salaam, ambazo wagombea waliahidi kuziboresha ndani ya kipindi kifupi, lakini ahadi hiyo haijatimia.

Kutotimiza ahadi kunazifanya baadhi ya barabara kuendelea kuharibika, huku wapigakura wakisubiri kile kilichoahidiwa na wabunge wao na huenda wanadhamini fedha za wabunge ndizo zinazotumika.

Binafsi ninajua kuwa kazi ya mbunge ni kuwakilisha wananchi kwa kupeleka bungeni kero za kimaendeleo zinazowakabili ili yaweze kupatiwa ufumbuzi, na hana uwezo wa kuwaletea maendeleo endelevu kwa kutumia fedha zake mwenyewe.

Hivyo, ni vyema mbunge akatoa ahadi na kufafanua jinsi atakavyoitekeleza, ili kuepuka lawama kutoka kwa wananchi, ambao huenda huamini kwamba mbunge anatumia fedha zake kuleta maendeleo jimboni.

Ninashauri hivyo kutokana na kwamba, wapo baadhi ya watu husifia wanapoona miundombinu mbalimbali imejengwa au kuboreshwa jimboni mwao, hushangilia na kusema vimefanywa na mbunge.

Lakini ukweli ni kwamba, mbunge hutia msukumo kwenye vyombo vya maamuzi kwa lengo la kuhakikisha kero za jimboni mwake zinapatiwa ufumbuzi kadri inavyowezekana.

Si vibaya wabunge wakakataa kubebeshwa mzigo usio wao, kwa kutoa ahadi ambazo wananchi huamini kwamba huenda watazitekeleza kwa kutumia fedha zao za mfukoni na kumbe sivyo.

Pamoja na hayo, ingependeza kama wananchi wanafundishwa kuhoji ili kwamba wanapokuwa kwenye kampeni, wapewe nafasi ya kuuliza ahadi za wagombea na jinsi watakavyozitekeleza.

Njia hiyo inaweza kupunguza ahadi zisizotekelezeka ambazo hutolewa na baadhi ya wagombea kwa lengo la kupata kura tu, na itakuwa rahisi kuwachuja na kupata wale ambao wataweza kuwaletea maendeleo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Msako vituo bubu vya mafuta uwe endelevu

**JUZI** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilitangaza kuanza msako wa kubaini wafanyabiashara wanaouza mafuta ya taa, dizeli na petroli bila leseni.

Lengo la msako huo ni kudhibiti matukio ya moto yanayoweza kutokea maeneo mbalimbali, ambayo baadhi yameshuhudiwa kuangamiza mali na maisha ya watu.

Uuzaji holela wa mafuta umekuwa tatizo sugu na sasa yanauzwa kama zinavyouzwa karanga au pipi kando kando ya barabara kuu.

Watu wanaouza mafuta hayo hawazingatii viwango vinavyotakiwa kuhifadhi mafuta hayo na badala yake huwekwa kwenye chupa za maji zilizotumika na kuwekwa kwenye jua.

Biashara hii imeshamiri hasa maeneo ya kando ya mji na wateja wakubwa ni waendesha bodaboda na bajaji ambao hununua rejareja kwa wafanyabiashara hao.

Kinachohatarisha zaidi ni mafuta hayo kuhifadhiwa ndani ya nyumba za kuishi watu bila kuchukua tahadhari ya moto. Vidumu hivyo vinawekwa sehemu ambazo moto unapotokea sio rahisi kuudhibiti na pia kuleta madhara kwa watu wengine wanaoishi jirani na nyumba zinazohifadhi mafuta hayo.

Akizungumza na vyombo vya habari juzi, Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, George Mhina, anasema kanda hiyo inaoongoza kwa matukio ya nyumba kuwaka moto unaosababishwa na uhifadhi wa mafuta ya petroli na dizeli kwenye makazi ya watu.

Anasema kuuza nishati hiyo bila utaratibu ni kinyume cha maelekezo ya mamlaka hiyo na kuwataka watu wanaofanya biashara hiyo wajisalimishe wenyewe kabla ya msoko huo haujaanza.

Mafuta ni kimiminika hatari ambacho hukifadhiwa kwenye matangi yanayochimbiwa ardhini, lakini wafanyabiashara wadogo wanauza mafuta kwenye chupa za maji ya kunywa kwa kuziweka nje juani hali ambayo inaweza kusababisha mlipuko na kuyafanya yakose ubora yanapotumiwa kwenye vyombo vya moto.

Ewura inatoa leseni kwa wafanyabiashara wanaomiliki vituo vya mafuta waliokidhi vigezo vya kisheria. Kwa wale wanaouza kwenye mapipa, madumu na chupa hawatakiwi kwa mujibu wa sheria.

Mamlaka hiyo imeweka utaratibu unaowataka wamiliki wa vituo vya mafuta vilivyopo mijini kujenga vituo vingine hususani vijijini ili kudhibiti wimbi la wauzaji wa mafuta wasio na leseni.

Pia inafafanua kuwa uwekaji wa vinasaba katika mafuta ya taa, petroli na dizeli kabla ya kuingia sokoni umesaidia kupunguza uchakataji wa nishati hiyo kwa asilimia 80 na kupunguza malalamiko yaliyokuwa yanawasilishwa EWURA kuwa mafuta ni machafu.

Ni imani yetu kuwa msako huo unaotarajiwa kuanza utamaliza kama sio kupunguza tatizo la uchakachuaji mafuta.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wapigakura wanachoka ahadi zisizotekelezeka

Na Sabato Kasika

**KILA** unapofanyika uchaguzi uwe wa urais, udiwani, ubunge hata umeya kuna ahadi kemkem zinazotolewa na wagombea kutoka vyama mbalimbali vya siasa kwenda kwa wapigakura kwa lengo la kuwashawishi na kuwavuta wamkubali.

Miongoni mwa ahadi hizo ambazo hutolewa na wanasiasa hao ujenzi au uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwamo ya barabara, madaraja, skimu za umwagiliaji na zahanati, lakini baadhi hazitekelezwi kulingana na jinsi walivyoahidi.

Inawezekana wapigakura wengi hushawishika kwa ahadi hizo za wakati wa kampeni bila kujua zinatekelezwa vipi, au ni fedha zipi zinazotumika kutekeleza ahadi hizo, badala yake hushangilia tu wanapoahidiwa.

Kutoelewa jinsi ya utekelezaji wa ahadi, kunaweza kuwafanya wagombea ubunge kupata kura kirahisi, kwa kuwa wanajua kwamba hata ikiwa ni ahadi hewa, wananchi hawana mwamko wa kuhoji.

Hivyo ingekuwa ni vyema wagombea wakawa wazi kuhusu jinsi ya kutekeleza ahadi wanazotoa wakati wa kampeni, kwamba watatumia fedha zipi kwa ajili ya kutekeleza ahadi hizo kuliko kuwaacha wananchi hewani.

Kwa wale wanaofuatilia siasa za Tanzania watakubaliana nami kwamba baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakitoa ahadi kwa wananchi ambazo matokeo yake huwa hawazitekelezi.

Mwanasiasa anaweza kuwa kwenye eneo ambalo lina ubovu wa barabara na kuahidi kwamba wananchi wakimchagua, atamaliza kero hiyo mara moja, hali ambayo huwafanya wamwamini, lakini badala yake ahadi hiyo haitekelezwi.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, wapo baadhi ya wagombea ubunge jijini Dar es Salaam waliotoa ahadi za kuboresha miundombinu ya barabara kwenye majimbo waliowania kwa kipindi kifupi.

Hata hivyo, unakaribia mwaka mmoja tangu kufanyika kwa uchaguzi, wengine hawajatekeleza ahadi hizo, waliahidi kuzimaliza ndani ya kipindi kifupi mara tu baada ya kuchaguliwa. Zipo barabara nyingi ambazo wanasiasa waliahidi kuziboresha, ikiwamo za majimbo ya wilaya ya Ubungo jijini Dar es Salaam, ambazo wagombea waliahidi kuziboresha ndani ya kipindi kifupi, lakini ahadi hiyo haijatimia.

Kutotimiza ahadi kunazifanya baadhi ya barabara kuendelea kuharibika, huku wapigakura wakisubiri kile kilichoahidiwa na wabunge wao na huenda wanadhamini fedha za wabunge ndizo zinazotumika.

Binafsi ninajua kuwa kazi ya mbunge ni kuwakilisha wananchi kwa kupeleka bungeni kero za kimaendeleo zinazowakabili ili yaweze kupatiwa ufumbuzi, na hana uwezo wa kuwaletea maendeleo endelevu kwa kutumia fedha zake mwenyewe.

Hivyo, ni vyema mbunge akatoa ahadi na kufafanua jinsi atakavyoitekeleza, ili kuepuka lawama kutoka kwa wananchi, ambao huenda huamini kwamba mbunge anatumia fedha zake kuleta maendeleo jimboni.

Ninashauri hivyo kutokana na kwamba, wapo baadhi ya watu husifia wanapoona miundombinu mbalimbali imejengwa au kuboreshwa jimboni mwao, hushangilia na kusema vimefanywa na mbunge.

Lakini ukweli ni kwamba, mbunge hutia msukumo kwenye vyombo vya maamuzi kwa lengo la kuhakikisha kero za jimboni mwake zinapatiwa ufumbuzi kadri inavyowezekana.

Si vibaya wabunge wakakataa kubebeshwa mzigo usio wao, kwa kutoa ahadi ambazo wananchi huamini kwamba huenda wanazitekeleza kwa kutumia fedha zao za mfukoni na kumbe sivyo.

Pamoja na hayo, ingependeza kama wananchi wanafundishwa kuhoji ili kwamba wanapokuwa kwenye kampeni, wapewe nafasi ya kuuliza ahadi za wagombea na jinsi watakavyozitekeleza.

Njia hiyo inaweza kupunguza ahadi zisizotekelezeka ambazo hutolewa na baadhi ya wagombea kwa lengo la kupata kura tu, na itakuwa rahisi kuwachuja na kupata wale ambao wataweza kuwaletea maendeleo.

## TAKUKURU yanusa ufisadi miradi 10

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU), mkoani hapa imenusa harufu ya ufisadi katika miradi 10 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 3.7.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapo, Hussein Mussa, alibainisha hayo jana wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kwa kipindi cha robo ya kwanza kati ya mwezi Julai hadi Septemba, mwaka huu.

Musa alisema baada ya uchunguzi wa kina katika miradi hiyo walibaini kuwapo upungufu na kuagiza yafanyike marekebisho ili iendane na thamani halisi ya fedha. Kadhalika, fundi pikipiki mkazi wa Kiloleli wilayani Kishapu, Onesmo Mwandu, amehukimiwa jela miaka mitatu baada kushindwa kulipa faini Sh. 500,000 kutokana na kupokea fedha za rushwa kutoka kwa mzazi ili kumsaidia kupata uhamisho wa mtoto wake.

"Katika kesi mbili ambazo tumeshinda moja ilihusisha watu wawili, akiwamo Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kiloleli wilayani Kishapu, Juma Kulwa, ambaye aliomba rushwa ya Sh. 100,000, kwa ajili ya kumsaidia mzazi Kasembe Lukarasha, kumhamisha mtoto wake katika shule nyingine," alisema Mussa.

"Mwalimu huyu hakuipokea fedha hiyo, badala yake alimtumia fundi pikipiki Onesmo Mwandu kuipokea kwa niaba yake na hukumu ilipotoka ya kwenda jela miaka mitatu au kulipa Sh. 500,000, mwalimu alilipa faini hiyo, lakini fundi pikipiki alishindwa ndipo akafungwa jela," aliongeza.

Aidha, Musa alisema katika kesi 21 za rushwa nne ziliamuliwa, mbili walishindwa huku wakishinda mbili na watuhumiwa kutiwa hatiani.

Alisema kesi nyingine walioshinda ni ya Edwini Mgeta, ambaye alijifanya ni Ofisa wa TAKUKURU na kwenda kufanya utapeli kwenye Idara ya Uhamiaji.

Katika kesi hiyo mtuhumiwa alihukumiwa kwenda jela miaka mitatu au kulipa Sh. 500,000 ambazo alilipa na kuachiwa huru.

Katika kipindi cha miezi mitatu, Musa alisema walipokea malalamiko 46 ya rushwa kutoka serikali za mitaa, elimu, ardhi madini, ujenzi, afya, siasa, fedha, biashara, mahakama, kazi, maliasili na barabara.

# NARCO yahamasisha ulaji wa nyama

**Na Beatrice Shayo**

KAMPUNI ya Ranchi za Taifa (NARCO), imewataka viongozi wa mikoa nchini kujenga utaratibu wa kufanya matamasha ya ulaji nyama ili kuhamasisha wananchi kuongeza wigo wa ulaji kama inavyotakiwa kila mwananchi kilo 50 kwa mwaka.

Meneja Masoko wa NARCO, Immanuel Mnzava, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa Tamasha la Nyama Choma Sumbawanga lilioandaliwa na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, lililokwenda sambamba na uanzishaji wa mnada katika kata ya Pito, Kijiji cha Katumba Azimio.

Alisema NARCO kama mdau mwalikwa kwenye tamasha hilo, inahamasisha ulaji wa nyama na hasa nyama ya Kongwa inayozalishwa na NARCO ambayo ina ranchi 14 nchini ikiwamo Ranchi ya Kalambo iliyoko mkoani Rukwa.

Mnzava aliongeza kuwa uhamasishaji huo unafanyika ili kuongeza ulaji wa nyama nchini. Alisema kwa mujibu wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), ulaji wa nyama nchini kwa mtu mmoja bado uko chini ambao ni wastani wa kilo 15 kwa mwaka tofauti na pendekezo la dunia la ulaji wa kilo 50 kwa mwaka unaopendekezwa.

Kwa mujibu wa Mnzava, wastani kila mwananchi ili afikie viwango vya ulaji nyama vinavyopendekezwa duniani inatakiwa kuongeza kilo 35 ili afikishe kilo 50 kwa mwaka.

Alisema matamasha ya ulaji nyama nchini yataongeza soko la ndani la bidhaa za mifugo na mazao, hivyo kutoa fursa kwa wananchi kufurahia rasilimali zinazozalishwa nchini katika sekta ya mifugo.

"Hili ni soko kubwa la ndani ikiwa Watanzania wote watakula nyama kulingana na viwango vinavyopendekezwa duniani. Tunapofanya matamasha kama haya, tuna lengo la kuhamasisha wananchi kuongeza ulaji wa nyama na wazalishaji wetu wa mifugo na mazao wanapata soko la mifugo yao na mazao yake ikiwamo nyama," alisema Mnzava.

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, alisema tamasha hilo ni moja ya vyanzo vya mapato na yatafungua fursa ya utalii wa ndani nchini.

Alisema uwapo wa NARCO ni sehemu ya kuliongezea pia thamani zao la ngozi kwa kuwa ulaji wa nyama ukiongezeka utasababisha pia uwapo wa ngozi za kutosha katika matumizi ya viwandani pamoja na chakula.

Baadhi ya watu walioshiriki katika tamasha hilo, walielezea kufurahishwa kwao na uwapo wa NARCO kwa kuwa imekuwa ikitoa mbegu bora za mifugo kwa maana ya ng'ombe, mbuzi na kondoo na mifugo hiyo imekuwa ikitoa nyama yenye ubora.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Zuberi Homera (kulia), akiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu (kushoto), baada ya kuwasili katika hafla ya chakula maalum kwa ajili ya wateja wa benki hiyo, mkoani humo juzi, iliyolenga kutoa wasaa wa kujadili fursa za kibiashara, mipango ya ukuaji na huduma zitolewazo na benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC akoshwa jitihada benki kuhudumia wafanyabiashara

**Na Mwandishi wetu**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameelezea kuridhishwa na huduma pamoja na jitihada za Benki ya Exim katika kuwahudumia wafanyabiashara na wateja wengine huku akionyesha kuvutiwa zaidi na riba nafuu inayotolewa na benki hiyo.

Homela alitoa kauli hiyo alipokuwa akizungumza kwenye hafla ya chakula maalum kwa ajili ya wateja wa benki huyo mkoani Mbeya ili kutoa wasaa wa kujadili fursa za kibiashara, mipango ya ukuaji na huduma zitolewazo na benki hiyo katika mkoa huo.

"Baada ya kufuatilia vizuri huduma za Benki ya Exim nimebaini kuwa ni huduma rafiki zaidi kwa wafanyabishara na wajasiriamali na zaidi nimevutiwa na kiwango cha riba kinachotozwa kupitia mikopo yao ambacho hakimuumizi mkopaji.

"Binafsi nimevutiwa zaidi na akaunti ya watoto pamoja na akaunti wa akiba na kudhihirisha hili nipo tayari kufungua akaunti hizi ili niweze kufurahia huduma hizi," alisema.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na wadau mbalimbali wa benki hiyo wakiwamo viongozi wa serikali, wafanyabiashara wakubwa na wadogo na wafanyakazi wa benki hiyo wakiongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Jaffari Matundu.

Awali, Matundu alisema kupitia tukio hilo muhimu, walilenga pia kutoa fursa miongoni mwa wateja hao ili kufahamiana na kufungua wigo wa kufanya biashara pamoja sambamba na wateja kufahamu huduma mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo.

Matundu alisema hali ya uchumi katika mkoa huo inatoa fursa kubwa ya ukuaji kwa benki hiyo ndiyo maana imejipanga kuhudumia wateja wakubwa, wadogo na wa kati ili kuleta ustawi kwenye sekta muhimu kwa mkoa huo zikiwamo biashara, kilimo na ufugaji.

Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa Exim, Andrew Lyimo, aliwatoa hofu wateja wa benki hiyo mkoani humo kuendelea kuiamini benki hiyo kwa kuwa imeendelea kujitanua zaidi hadi nje ya mipaka ya Tanzania ikiwamo Uganda, Ethiopia, Comoro na Djibouti.

"Ni kupitia kujitanua kwetu huku hadi nje ya mipaka ya nchi, ndiyo sababu tunawakikishia wateja wetu kwamba hakuna haja ya kujifungia ndani ya mipaka yetu ni wao tu kufungua milango hadi nje ya mipaka kwa sababu Exim tuko nao hadi nje ya mipaka.

"Zaidi, tumejipanga kuhakikisha benki inafanya vizuri kwa kuweka kipaumbele katika uboreshaji wa namna ya kupata na kutumia huduma zetu. Tunataka upatikanaji na utumiaji wa huduma za Benki ya Exim uwe rahisi, huku tukiendelea kusizogeza huduma hizo karibu zaidi na wateja wetu," alisema.

# Waziri aagiza utafiti usonji

Na Beatrice Shayo

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameagiza taasisi za serikali na zisizo za kiserikali kufanya utafiti kuhusu tatizo la usonji nchini.

Amesema kwa kufanya hivyo kutasaidia upatikanaji wa huduma kwa watoto wenye ugonjwa huo.

Gwajima alitoa agizo hilo juzi wakati wa hafla ya uelimishaji jamii kuhusu usonji iliyoandaliwa na taasisi inayojishughulisha na masuala ya usonji ya Lukiza Autism Foundation.

Alisema utafiti huo uwekwe wazi na serikali itatoa ushirikiano kuhakikisha unafanyika na matokeo yanatumika kuimarisha huduma kwa watoto wenye usonji nchini.

Kwa mujibu wa waziri, ni muhimu kwa Tanzania kuwapo kwa takwimu halisi zinazoonyesha watoto wenye usonji ili wapatiwe huduma bila kuathiri hali ya wazazi kiuchumi.

"Jambo hili limenigusa na limenifungua na limenipa mtihani wa kwenda kujipanga upya katika sekta yangu na wadau wote nikitoka hapa, ili tuwe na timu ya kitaifa ya kulitazama jambo hilo kwa kina," alisema.

Waziri alisema wasipotazamwa wenye usonji itakuwa mzigo kwa serikali kwa kuwa wakiwezeshwa wanaweza kufanya mambo makubwa ya maendeleo kuliko hata hao wanaodai ni wazima.

Aliagiza kabla ya Novemba 30, mwaka huu, kufanyike kikao cha wadau kutazame na kutengeneza kamati ya wataalamu wa sekta hiyo kwa ajili ya kupata muafaka wa vitu muhimu vya kuwasaidia watoto wenye usonji.

"Nimebaki najiuliza kila siku tunapata takwimu za afya kutoka kwenye vituo vyetu ina maana hawa watoto huwa hawaumwi mbona takwimu zake huwa sizioni kuna kitu akipo sawa ama wanaenda hawagunduliki ama wanagundulika hawaripotiwi," alisema.

Waziri alisema kama taarifa zao hazijulikani mipango ya maendeleo yao haiwezi kuonekana hilo ni jambo kubwa linatakiwa kuangaliwa kwa umakini na endapo lisipoangaliwa kuna uwezekano watakapozeeka likawepo kwa taifa lenye watu wengi wa usonji.

Pia amewataka wataalamu wa afya nchini kutoa elimu ya ugonjwa wa usonji kwa jamii itaisaidia kwa kiasi kikubwa kuwa na uelewa na kuachana na imani potofu.

"Nitoe rai kwa wataalamu wetu wa afya na elimu au wawakilishi wao, madaktari, ustawi wa jamii, kutumia elimu na uelewa uliopatikana kuhusu usonji kwa kuwaelimisha wengine ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii," alisema.

Waziri alisema takwimu zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2020 zinaonyesha kuwa katika kila watoto 132 duniani, mmoja ana usonji, hivyo kusisitiza kutolewa kwa elimu zaidi ili kuwa na jamii yenye uelewa wa kutosha.

"Tanzania, takwimu zilizopo ni za idadi ya watoto wenye usonji waliofanyiwa usaili katika shule maalum na wale walioonwa katika vituo vya kutolea huduma, takwimu za mwaka 2018 zinaonyesha kuwa, wanafunzi 1,416 wana usonji na walimu 157 katika shule 18 za msingi," alisema.

Aidha, Dk. Gwajima alitoa rai kwa wataalamu wa afya na elimu wakiwamo madaktari, maofisa ustawi wa jamii, walimu wa watoto wenye uhitaji maalum na waandishi wa habari waliopata fursa ya kushiriki katika hafla hiyo, kutumia ujuzi huo kuwaelimisha wengine, ili kuepuka unyanyapaa dhidi ya watu wenye changamoto hiyo.




Mkuu wa Wilaya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija (kulia), akiwa na mshindi wa Sh. milioni 10 wa bahati nasibu ya Biko, Eugine Paullo Mbassa (katikati), wakati wa makabidhiano ya fedha hizo katika tawi la Benki ya NBC Viwandani, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Balozi wa Biko, Kajala Masanja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yatangaza washindi kampeni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani'

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) jana iliwatangaza washindi wa droo ya kwanza katika promosheni yake ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani' inayolenga kuwahamasisha wakulima wa korosho katika mikoa ya Lindi na Mtwara kujiunga kwa kufungua akaunti ya NBC Shambani.

Akaunti hiyo inatajwa kuwa na faida nyingi kwa mkulima na vyama vya ushirika ili kujikwamua kutoka kwenye changamoto mbalimbali za huduma za kifedha zinazokwamisha jitihada zao za kujikwamua na umaskini kupitia kilimo cha zao hilo.

Akitangaza washindi kwenye droo ya kwanza iliyofanyika Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo, Lariba na Wakulima kutoka NBC, Raymond Urassa, alisema washindi 26 walipatikana kupitia droo hiyo wakijishindia zawadi mbalimbali zikiwamo baiskeli, pikipiki, pampu za kupulizia dawa mikorosho, guta (Toyo), kanga, mabegi ya shule na madaftari.

"Kupitia droo hii leo washindi wamepatikana katika makundi ya mkulima mmoja mmoja na kupitia vyama vya msingi (AMCOS). Kupitia kundi la kwanza ambalo ni mkulima mmoja mmoja washindi 10 wamejishindia baiskeli kila mmoja, huku pia washindi wengine watano wakijishindia pikipiki kila mmoja. Washindi wengine 10 nao wamejishindia pampu za kupulizia dawa kila mmoja. Upande wa AMCOS mshindi ni AMCOS ya Mpindimbi iliyoko wilayani Masasi iliyojishindia zawadi ya Toyo moja."

"Washindi hawa watakabidhiwa zawadi zao kila wiki. Ili walengwa hawa wote waweze kujishindia zawadi hizi, wanatakiwa wafungue akaunti ya NBC Shambani na wapitishe fedha za malipo ya mauzo yao ya korosho kwenye akaunti hizo na moja kwa moja watakuwa wameingia kwenye droo ya kujishindia zawadi hizi," alisema.

Urassa alisema benki hiyo itaendelea kutimiza ahadi ya kuwapatia washindi wa kampeni hiyo zawadi hizo na kwamba zawadi hizo zinalenga kuwasaidia kutimiza ndoto zao kupitia kilimo cha zao la korosho.

Promosheni hiyo ya mizezi mitatu ilianza rasmi katikati ya mwezi Septemba mwaka huu na inatarajia kufikia tamati mwanzoni mwa Januari.

Ofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Jorum Mtafya, alitoa pongezi kwa washindi wa promosheni hiyo huku akiwahamasisha walengwa kushiriki kwa wingi na kwamba wana nafasi kubwa ya kujishindia zawadi katika droo zinazofuata.

# Chato yasimamisha likizo za watumishi

Na Daniel Limbe, CHATO

SERIKALI wilayani Chato mkoani Geita imesitisha likizo za watumishi wake katika kipindi chote cha msimu wa kilimo cha mwaka 2021/2022.

Kadhalika, imefuta barua zote za maofisa ugani wa halmashauri hiyo (hakuwataja) waliotaka kuhamia Bodi ya Pamba Nchini (TCB), kwa lengo la kusimamia uzalishaji wa zao hilo.

Uamuzi huo ulichukuliwa jana mjini hapa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Mandia Kihiyo, baada ya kupokea ushauri wa kitaalamu kutoka kwa Balozi wa zao la pamba nchini, Agrey Mwanry.

Mwanry alikuwa katika majumuisho ya mikutano yake iliyolenga kuhamasisha kilimo cha pamba kwa wakulima wa wilayani humo, baada ya takwimu kuonyesha uzalishaji huo kushuka kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na awali.

Kwa mujibu wa takwimu za uzalishaji wa zao hilo kwa msimu wa kilimo wa 2020/2021, halmashauri hiyo ilizalisha tani 2,600 kinyume na malengo ya tani 16,000 baada ya mwamko wa wakulima kushuka kutokana na bei, ongezeko la wadudu waharibifu pamoja na kilimo cha mazoea.

Alisema kutokana na elimu iliyotolewa kwa wakulima hao, kuna uwezekano wa zao hilo kurejea kwenye hadhi yake na kwamba jukumu kubwa lililobaki ni kwa maofisa wa serikali kuanzia tarafa, kata na vijiji kuwasimamia ipaswavyo wakulima wao.

Mwanry alishauri serikali kusitisha likizo za baadhi ya watumishi ili waongeze kasi ya kuelimisha wakulima kuzingatia kanuni bora za kilimo cha pamba kuanzia maandalizi ya shamba, kutumia mbolea, kupanda kwa nafasi, kupalilia na kuvuna kwa usafi ili kuongeza thamani ya zao hilo.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo alitangaza kusitisha likizo zote za maofisa ugani pamoja na kuzifuta barua zaidi ya 10 za watumishi walioomba kuhamia TCB ili kwenda kuwa wakaguzi wa zao hilo.

Alisema hatua hiyo itasaidia kufikia malengo yaliyowekwa na mkoa ya kuzalisha tani 35,000, kwa msimu wa kilimo wa 2021/22 ikilinganishwa na malengo ya tani 16,000, kwa msimu uliopita.

Wakati uamuzi huo ukifikiwa Mkuu wa Wilaya ya Chato, Martha Mkupasi, alitaka watendaji kutumia sheria zilizopo kuwatoza faini wakulima ambao bado hawajaondoa maotea ya pamba kwenye mashamba yao.

# Hatimaye wakulima waiangukia serikali

Na Elizabeth John, MBEYA

WAKULIMA 3,800 wa mpunga kutoka Bonde la Mnazi lililoko wilayani Mbarali, mkoani Mbeya wameiomba serikali kuangalia namna bora ya kutatua mgogoro wa ardhi baina yao na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Ombi hilo limetolewa hivi karibuni na wakulima wanaotumia eneo hilo wakiwamo umoja wa nguvu kazi Mwanavala, ambao wamekuwa na wasiwasi na kauli ya serikali kuhusu kufanya mapitio upya ya GN namba 28 inayohusisha vijiji 31 vilivyopo wilayani Mbarali.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwa niaba ya wenzao, Upendo Kyambiki na Shabani Nguluvala, walisema kwa miaka mingi wanalima mpunga kwenye bonde hilo, na kwamba kutaka kuwaondoa jirani na eneo la Ihefu kutasababisha kushindwe kumudu maisha yao.

Walisema wanategemea kilimo kwa shughuli zao za kujiingizia kipato cha familia na kwamba wakiondolewa eneo hilo watakosa pa kwenda na taarifa aliyopelekewa Rais Samia Suluhu Hassan kuwa wako wachache sio za kujenga bali kuwaumiza.

"Sisi tumezaliwa Mbarali maisha yetu yote ni hapa hata makaburi ya ndugu zetu yapo hapa sasa tukifukuzwa tutaenda kuishi wapi tunaomba Rais asikie kilio chetu," alisema Upendo.

Naye Irene Ngailo, aliiomba serikali kuangalia namna bora ili wakulima waweze kuwa salama sambamba na kuendelea na kilimo hicho.

Mmoja wa viongozi wa umoja wa wakulima wa zao la mpunga wilayani Mbarali, Athanasi Kikwembe, alisema walipeleka rasimu inayoonyesha mahitaji ya mkopo wa fedha ya Sh. bilioni 3.1 kupitia eneo hilo sasa kitendo cha kutaka kuwaondoa kwenye eneo hilo ni kutowatakia mema.

Akizungumza kwa njia ya simu, Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema alikwenda mkoani Mbeya ili kutembelea maeneo yote ya mkoa huo ambayo yana mwingiliano na maeneo ya hifadhi.

Alisema kulingana na maagizo ya Rais wameunda timu ya kufanya tathmini ambayo haitoleta taharuki kwa wananchi kwa kuzingatia maslahi mapana ya taifa.

# Chanjo corona yasaidia kurudisha biashara utalii

Na Christina Haule, MBEYA

WATENDAJI wa huduma za hoteli jijini hapa wamepongeza hatua ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwezesha nchi kupata chanjo ya kujikinga na mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Uviko-19 na kurejesha hali nzuri kibiashara katika sekta ya utalii na uwekezaji.

Wamesema hatua hiyo imewezesha kuondoa athari zilizojitokeza kutokana na mlipuko huo na sekta ya utalii kwa ujumla ikiwamo hoteli na nyumba za kulala wageni kuathirika kwa kukosa wageni.

Wamiliki hao walisema hali hiyo kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na kundi la waandishi wa habari zaidi ya 30 wanaofanya ziara ya kutangaza vivutio vya utalii na uwekezaji nchini wakimsapoti Rais Samia katika kutangaza vivutio hivyo.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Usungilo ambao pia ni wamiliki wa Hoteli ya Usungilo, Kata ya Forest jijini hapo, Hotman Nyagawa, alisema ujio wa chanjo ya Uviko-19 imewezesha sekta ya utalii kuanza kurejea katika hali yake ya kawaida kwa upatikanaji wa wateja.

"Mwaka 2020/21 sekta ya utalii ikiwamo hoteli na nyumba za kulala wageni tuliathirika kwa kiasi kikubwa, hali ilikuwa mbaya hatukuwa tukipokea wageni pia sisi kwa sisi tulikuwa tunaogopana, tunamshukuru sana Rais, Samia kwa kuwezesha nchi kupata chanjo watu wamechanga na hivi sasa wanaendelea na shughuli zao kama kawaida," alisema.

Alisema kwa sasa angalau wanakusanya japo asilimia 30 ya mapato tofauti na wakati wa corona walilazimika kufunga kutokana na biashara kuwa mbaya.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa Hoteli Desderia, William Jima, alisema wameweza kuchangia katika sekta ya utalii kwa kuajiri asilimia 98 ya vijana kutoka Mkoa wa Mbeya na nje ya mkoa huo.

Kuhusu athari za Uviko-19 alisema waliathirika kwa kiasi kikubwa baada ya mlipuko huo, lakini kwa sasa hali imebadilika na wageni wameanza kuingia kama kawaida.

"Nawashauri watu wakachanje ili maisha yaweze kuendelea kwani ukichanja unakuwa umejikinga na mlipuko wa Uviko-19, tusipuuze kuchanja maana ni kawaida yetu, japo kuchanja ni hiari," alisema.

Hivi karibuni Rais, Samia amezindua kampeni ya kuchanja kwa hiari inayoendeshwa nchi nzima na kila wizara sambamba na kutoa mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), kwa ajili ya mapambano dhidi ya Uviko-19 na kupunguza athari zilizotokana na ugonjwa huo.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa daraja linalounganisha eneo la Mbezi Louis na Kitongoji cha Mshikamano katika Mto Mbezi, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana, litakalopunguza usumbufu kwa wananchi hasa nyakati za mvua. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Utekelezaji mpango miaka 5 ujenzi shule 1,000 kuanza

Na Augusta Njoji, DODOMA

UTEKELEZAJI wa mpango wa miaka mitano wa ujenzi wa shule mpya 1,000 za sekondari nchini unatarajiwa kuanza hivi karibuni na unalenga kata ambazo hazina shule na zenye idadi kubwa ya wanafunzi.

Pia zitajengwa shule 26 za wasichana kila mkoa kwa ajili wanafunzi watakaofaulu kuingia kidato cha tano na sita ili kusoma bila kikwazo na kufikia ndoto zao.

Akizungumza wakati wa kufungua mafunzo ya kuwajengea uwezo, wataalamu wa Idara ya Elimu, Maofisa Maendeleo ya Jamii, Wahandisi na Maofisa Mazingira, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Gerald Mweli, alisema ujenzi huo unafanyika chini ya Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kwa fedha za mkopo wa Dola za Marekani milioni 500 sawa na Sh. trilioni 1.1 kutoka Benki ya Dunia (WB).

Alisema mradi huo unalenga maeneo ya utoaji elimu nje ya mfumo rasmi, uimarishaji wa ujifunzaji na ufundishaji, ujenzi wa miundombinu na kupunguza vikwazo kwa wasichana kujenga mabweni na kutoa elimu ya unasihi na nasaa katika shule ili kuwa na uhakika watoto wanakuwa wakiwa wanafahamu kero zinazowazunguka.

Alisema serikali imejipanga ifikapo mwaka 2023 malengo ya SEQUIP yawe yametekelezwa.

"Kama mnavyofahamu ujenzi wa shule au miundombinu umekuwa na changamoto nyingi sana za uharibifu wa mazingira, tumejipanga serikali pamoja na wafadhili wa maendeleo tunapokwenda kutekeleza mpango wetu wa kuinua elimu ya sekondari kwa miaka mitano, lakini tulinde mazingira," alisema.

Alisema kufanyika kwa kikao na wataalamu hao ni maandalizi ya kuanza kutekeleza mradi huo.

"Tumeandaa kikao hiki cha wataalamu kwa ajili ya kuhakikisha miongozo ya utekelezaji inafuatwa na kusimamiwa, pia tunajenga shule moja kila mkoa tumeandaa michoro kwa ajili ya shule hizi, lakini pia michoro hii imeambatanisha na miongozo ya jinsi gani wakati wa utekelezaji tutashirikisha jamii, kusimamia wakandarasi na mafundi kutekeleza mradi na mazingira yanatunzwa," alisema.

Aliwataka kusimamia vyema utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwa ni jukumu zito na deni kwa taifa.

"Ndio maana tumewaita Maofisa wa Maendeleo ya Jamii kwa mara ya kwanza katika utekelezaji wa mradi hautakuwa unamilikiwa na maofisa elimu pekee bali Wahandisi watakuwa na sehemu yao, maofisa ustawi wa jamii na maofisa mazingira," alisema.

Aliwataka kuhakikisha mikataba ya mafundi au wakandarasi inakuwa na miongozo ya maadili ya kazi na wanajengewa uwezo baada ya kuanza ujenzi na kuzingatia viwango vya majengo husika.

"Mara nyingine tunapewa ardhi na kijiji, taratibu hazijakamilishwa wakati wa utekelezaji wanakuja wanakijiji wanasema tumenyang'anywa eneo letu au hatujalipwa fidia jambo hili hatulitegemei ilitokee wakati wa utekelezaji," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Usimamizi wa Elimu kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Ephraimu Sembeye, alisema kikao hicho kina washiriki 630 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

# Bunge latoa msimamo kupanda bei ya mbolea

BUNGE limeitaka serikali kutoa taarifa ya kina bungeni ya kunusuru tatizo la kupanda kwa bei ya mbolea.

Hata hivyo, serikali imesema bei za mbolea katika msimu wa 2021/22 zimeendelea kupanda katika soko la dunia kutokana na athari za Uviko-19 zilizochangia kushuka kwa uzalishaji viwandani na vingine kusimamisha.

Aidha, baadhi ya nchi wazalishaji wa mbolea wamesimamisha biashara ya mbolea nje ya nchi zao ili kutosheleza mahitaji yao.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alitoa agizo hilo jana bungeni kabla ya Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Stella Fiyao, kuuliza swali ambalo alilenga kujua serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na bei kubwa ya mbolea nchini.

Ndugai alisema swali hilo ni zito la Bunge zima na kwamba wanatarajia serikali itakuja kutolea ufafanuzi suala hilo kutokana na bei kupanda kutoka wastani wa Sh. 55,000 hadi 60,000 ya mwaka jana na kufikia Sh. 110,000 hadi 120,000.

"Bei ambayo wakulima wetu kwa vyovyote vile hawawezi kumudu, na ikiendelea na Mamlaka ya Hali ya Hewa wanatuambia mwaka huu mvua zitakuwa za wastani sana na mbolea hakuna tunaweza kuwa na janga kubwa sana la njaa mwakani."

"Jambo hili ni kubwa na tunataka serikali iangalie kwa undani wake na kabla Bunge hili halijaisha tutapata maelezo ya kutosha kuhusu jambo hili kwa sababu ni zito," alisema.

Katika majibu ya Wizara ya Kilimo kwenye swali hilo, yalieleza kuwa bei ya mbolea ya kukuzia aina ya Urea imepanda kutoka Dola za Marekani 310 msimu wa 2020/21 hadi Dola za Marekani 570 kwa tani kwa mwezi Septemba, 2021.

Aidha, wizara ilisema mbolea ya kupandia aina ya DAP imepanda kutoka Dola za Marekani 410 msimu wa 2020/21 hadi Dola za Marekani 806 kwa tani kwa mbolea iliyoingizwa mwezi Septemba, 2021.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, serikali imeendelea kutekeleza mikakati ya muda mrefu na mfupi.


Ilitaja mikakati hiyo kuwa ni kutafuta mbolea kupitia Ofisi za Ubalozi wa Tanzania katika nchi wazalishaji wa mbolea kama vile Misri, Saudi Arabia, Urusi, Algeria, China na Morroco ili kupata mbolea itakayonunuliwa na serikali kupitia Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) na kuiuza kwa wakulima kwa bei nafuu.

Pia ilisema kuruhusu wafanyabiashara kuingiza mbolea nchini bila kulazimika kutumia utaratibu wa zabuni za Mfumo wa Ununuzi kwa pamoja (BPS) ili kuuza kwa bei ya ushindani na kati ya Julai hadi Septemba, 2021 jumla ya tani 178,800 zimeingizwa nchini ikilinganishwa na tani 54,964 pekee za mbolea ambazo zingeingizwa nchini kwa mfumo wa BPS.

Kadhalika, ilisema kuhamasisha matumizi ya mbolea zenye bei nafuu ambazo ni mbadala wa DAP na UREA kama vile NPK, NPS, NPS-Zinc, Minjingu, FOMI, mbolea za asili na chokaa na kutoa kipaumbele cha uondoshaji wa shehena ya mbolea kwa meli zote zinazoingiza ili kuepuka gharama za kukaa bandarini.

Ilisema mkakati wa muda mrefu ni pamoja na kuendelea kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya mbolea ikiwamo kuongeza uzalishaji wa kiwanda cha Minjingu kutoka wastani wa tani 28,000 hadi 100,000 kwa mwaka.

Vilevile, ilisema Kiwanda cha Itracom Fertilizer Ltd kimeanza kujengwa katika eneo la Nala, jijini Dodoma kitakachokuwa na uwezo wa kuzalisha tani 600,000 za mbolea kwa mwaka.



Spika wa Bunge, Job Ndugai akimwapisha Mbunge mpya wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani (kushoto), katika kikao cha kwanza cha Bunge la Tano, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mipaka nchini kuboreshwa 2022/23

WIZARA ya Fedha na Mipango imesema kwa mwaka 2022/23 imepanga kuboresha mipaka mbalimbali nchini ikiwamo ya Kirongwe ili taasisi za serikali zitoe huduma kwa pamoja. Naibu Waziri wa wizara hiyo, Hamad Yusuf Masauni, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Rorya (CCM), Jafari Chege.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itaboresha mpaka wa Kirongwe kwa kujenga One Border Post (kituo cha huduma kwa pamoja) ili kuimarisha na kuongeza mapato ya serikali.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Masauni, alisema serikali ina mpango wa kuboresha mpaka wa Kirongwe kwa kuweka miundombinu wezeshi itakayotoa huduma kwa pamoja.

Vile vile, alisema katika mwaka 2021/22, serikali imetenga Sh. milioni 407 kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa nyumba za makazi za watumishi Kirongwe.

Pia itaendelea kuimarisha mipaka kwa kujenga nyumba za makazi kwa watumishi wa taasisi zinazofanya kazi mipakani na ofisi za kutolea huduma kwa pamoja mipakani ili kuboresha ulinzi na usalama wa nchi na kuongeza mapato serikalini.




Habari zote na Augusta Njoji

## Serikali kutafuta soko la tumbaku nje

SERIKALI kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania imejipanga kutafuta masoko ya tumbaku nje ya nchi na kuwashawishi wanunuzi waliopo kuongeza kiwango cha ununuzi kwa njia ya mkataba.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe aliyasema hayo bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Sikonge (CCM), Joseph Kakunda.

Katika swali lake, Kakunda alihoji lini serikali itamaliza tatizo sugu la soko la zao la tumbaku nchini.

Akijibu swali hilo, Bashe alisema soko hilo linategemea mahitaji katika soko la dunia ambalo mahitaji ya tumbaku na bidhaa zake yamekuwa yakishuka katika soko la dunia kwa wastani wa asilimia sita hadi saba kwa mwaka.

Alisema hali hiyo inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kampeni ya kidunia ya kupunguza uzalishaji na matumizi ya tumbaku pamoja na bidhaa zake, pamoja kuanza matumizi ya sigara aina mpya inayotumia kilevi cha kutengeneza maabara iitwayo e-cigarette.

Hata hivyo, alisema kutokana na hatua mbalimbali za serikali, wanunuzi wakubwa wameongeza ununuzi wa tumbaku kutoka kilo milioni 39 msimu wa mwaka 2017/18 na kufikia kilo milioni 57 msimu wa mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 46.

"Serikali imehamasisha wanunuzi wapya na kwa msimu wa kilimo 2020/21 kampuni nane za kizawa zilingia mkataba na wakulima kununua kilo milioni 17," alisema.

Katika hatua nyingine, alisema serikali imeendelea kutafuta masoko mapya na inaendelea kutafuta soko la China ambao walileta aina ya tumbaku wanayotaka na majaribio yamefanyika na sampuli yake imepelekwa kwa hatua zaidi.

"Jitihada za kutafuta masoko zinaendelea katika nchi mbalimbali, serikali inaamini kuwa baada ya muda mfupi tatizo la soko kwa wakulima wa tumbaku wa Tanzania linaenda kupungua," alisema.

## Mwaka 1 wa Mwinyi Zanzibar...

Ukurasa 12






Ukurasa 13

**MIEZI SITA YA RAIS SAMIA**

**Undani wa ufanisi wake kuelekea kileleni miaka 60 Uhuru wa nchi**



# ACT-Wazalendo yaibuka na nguvu mpya

## ▮Kukoleza moto katiba mpya, tume huru



Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Juma Haji Duni ambaye nafasi yake iko wazi baada ya kujiuzulu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

KATIKA jitihada za kukoleza moto wa kusaka katiba mpya na tume huru ya uchaguzi kabla ya 2025, Chama cha ACT Wazalendo, kimetangaza kuungana na vyama vingine kupigania ajenda hizo.

Ni msimamo wa Halmashauri Kuu ya ACT-Wazalendo, iliyokutana jijini Dar es Salaam na kuazimia kuongeza kasi zaidi kudai katiba mpya na tume huru ya uchaguzi pamoja na sheria bora za uchaguzi.

Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Mahusiano ya Umma wa chama hicho, Janeth Rithe, anasema, anapozungumza na Nipashe.

Anasisitiza kuwa wanataka uchaguzi mkuu ujao wa 2025 uwe huru, wa haki na wakuaminika na unaokubalika na wadau wote.

"Chama kitaendelea kwa kasi zaidi kupigania katiba mpya na tume huru ya uchaguzi, hivyo kitakuwa mstari wa mbele kusimamia mageuzi ya kiuchaguzi ili uwe na sifa na vigezo vinavyokubalika na wadau wote ," anasema Janeth.

Chama hicho kinatangaza kuongeza kasi zaidi katika madai hayo, huku kwa upande wa CUF, kikiwa tayari kimeshatangaza kususa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 hadi taifa litakapopata katiba na tume huru ya uchaguzi.

Msimamo huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Taifa wa CUF, Profesa Ibrahim Lipumba, mara tu baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na kwamba kuanzia wakati huo chama hakitashiriki tena uchaguzi wowote.

Hadi hakijabadili msimamo huo, hali inayoonyesha kwamba kimedhamiria kudai uwepo wa katiba mpya na tume hiyo ambayo kinaamini inaweza kusimamia kikamilifu uchaguzi.

Chama kingine ambacho kimekuwa kikidai katiba mpya na tume huru ya uchaguzi ni CHADEMA, ambacho mwanzoni mwa mwaka huu kilitaka kufanya makongamano ya kufanikisha madai hayo.

Pamoja na hayo, baadhi ya wadau wametoa maoni yao ambayo wanaamini kwamba yanaweza kusaidia vyama vya upinzani kufanikisha upatikanaji wa katiba mpya na tume hiyo.

Miongoni mwa wadau hao ni mwanasheria na Dk. Hellen Kijo-Bisimba, Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, (LHRC) ambaye anaelezea mtazamo.

### MJADALA KITAIFA

Dokta Hellen, anawashauri wanasiasa kuwa tayari kuandaa utaratibu wa kuanzisha majadiliano na kiongozi wa nchi kuhusu hoja zao hizo, kwa kuwa suala la kuwapo katiba mpya na tume huru ni kwa faida ya Watanzania wote.

"Upinzani unadai katiba ya mwaka 1977 imepitwa na wakati ingawa imefanyiwa mabadiliko kadhaa, lakini wanaamini kuwa inatoa upendelea kwa chama kimoja. Njia bora ni kuanzisha majadiliano," anasema Dk. Bisimba.

Anasema, anakumbuka katika ilani ya CCM ya uchaguzi ya mwaka 2015 -2020 iliweka kipengele cha kuendelea na mchakato wa kuandaa katiba mpya, lakini baadaye kikawa kimeondolewa.

"Lakini kimsingi ni kwamba, katiba ni takwa la kisheria, hivyo ni kuwapo kwa mchakato bora ambao utawezesha ipatikane, hasa kwa kuanzisha majadiliano na Rais ili hatimaye kufikia muafaka," anasema.

Anasema, kasi ambayo ACT-Wazalendo imetangaza ingelenga kwenye majadiliano, kwa kuwa hayo ndiyo husaidia kuleta mwafaka katika mkwamo wa jambo lolote katika jamii na hata taifa.

### HAKUNA KUSUSA

Mjumbe wa Baraza la Jukwaa la Katiba Tanzania, Hebron Mwakagenda, anasema, chama kususa uchaguzi si njia sahihi, kwa maelezo kuwa kikisusa, vingine vitaendelea kushiriki kama kawaida.

"Njia nzuri ni kuendelea kudai kwa mbinu mbalimbali kuanzia kushawishi watawala kuitisha vikao vya pamoja ili hatimaye kufikia muafaka badala ya kutumia nguvu na wakati mwingine kusababisha madhara," anasema.

Mwakagenda anatolea mfano maandamano ya kudai katiba au tume huru, ni lazima vyama vijitathmini kwanza kuwa vina wanachama wangapi, wa aina gani kama wanaweza kukabiliana na mikikimiki.

"Pamoja na hayo yote, katiba mpya na tume huru ya uchaguzi ni vya muhimu, ndiyo maana mbunge wa Mtama CCM, Nape Nnauye, aliwahi kusema anatamani atangazwe na tume huru ya uchaguzi anapowania nafasi za kisiasa za kuchaguliwa," anasema Mwakagenda.

Anasema, Jukwaa la Katiba linatambua umuhimu wa hayo yote na kusisitiza kuwa njia sahihi ni kila chama kupaza sauti, huku kikishiriki katika uchaguzi badala ya kususa au kudai kwa mbinu zinazoweza kusababisha madhara.

"ACT-Wazalendo wanasema wataongeza kasi zaidi kufanikisha jukumu hilo, ila hawakufafanua kasi hiyo ni ya aina gani, lakini makongamano kama ambayo CHADEMA walikuwa wanataka kufanya ni mazuri," anasema.

### MRITHI WA MAALIM

Wakati kikipanga kuongeza kasi ya kudai hayo, ACT-Wazalendo pia kinajiandaa kufanya uchaguzi mkuu kwa ajili ya kuziba nafasi ya aliyekuwa mwenyekiti wa chama hicho taifa, Maalim Seif Shariff Hamad.

Nafasi hiyo ya mwenyekiti wa chama taifa iko wazi kufuatia kifo cha mkongwe huyo wa siasa za Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, aliyefariki mwanzoni mwa mwaka huu.

Kwa mujibu wa Rithe, uchaguzi huo utafanyika mwishoni mwa Januari mwaka ujao, pia ukihusisha kuziba nafasi mbalimbali ikiwamo ya Katibu Mkuu wa chama hicho, Juma Haji Duni aliyejiuzulu.




Rais Dk. Hussein Mwinyi alipoihutubia Zanzibar, amefikisha mwaka mmoja sasa katika uongozi wake. **PICHA: MTANDAO**

# Mwaka mmoja Rais Mwinyi Z'bar

## Yajaa manukato ya maridhiano, upatanisho, Pemba sasa ni raha

**Na Rahma Suleiman,**

**ZANZIBAR**

JANA Novemba 2, Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametimiza mwaka mmoja tangu alipoapishwa kuiongoza Zanzibar baada ya uchaguzi mkuu wa 2020.

Siku 365 Ikulu kwa Dk. Mwinyi zina mengi ya kujivunia ambayo yamepatikana ndani ya mwaka mmoja ya uongozi wake.

Ajenda kubwa ya mafanikio yake iko kwenye kuleta maridhiano ya kisiasa visiwani Zanzibar ambapo miaka ya nyuma kabla ya uongozi wake maridhiano hayo yalitetereka.

Kwa nyakati tofauti katika kipindi cha harakati za kampeni za kisiasa mwaka 2020, Dk. Mwinyi, anasisitiza kuwa hafurahishwi na mivutano ya kisiasa iliyopo visiwani humo wakati huo ambao athari zake ni kubwa kijamii na kiuchumi.

'Nikichaguliwa kuwa rais wa Zanzibar nitarudisha amani na utulivu uliopo na kuondoa siasa za chuki na uhasama ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikirudisha nyuma maendeleo ya kijamii na uchumi. Zimesababisha migogoro na chuki," ananukuliwa akisema Dk. Mwinyi.

Anayasema hayo kipindi hicho akigombea urais kwa tiketi ya CCM.

Hawakukosea wahenga waliosema kuwa ahadi ni deni hivyo kutokana na msimamo wa kuwa mpatanisho msemo huo wa wahenga, ulitimia Rais Mwinyi baada ya kupata ridhaa ya kuiongoza Zanzibar alilipa deni kwa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) na kusaidia kuondoa na kupunguza mihemko ya kisiasa.

Ingawa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilikuwapo kabla ya uongozi wa Dk. Mwinyi, ilitetereka baada ya kufutwa kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 na kufanyika tena uchaguzi wa marudio mwaka 2016 ambapo chama kikuu cha upinzani kwa wakati huo CUF hakikushiriki.

Hapo ndipo SUK ilipoanza kutetereka na Zanzibar kuendelea kuongozwa na chama kimoja pekee cha CCM ambacho kilishinda kwa asilimia 99 katika uchaguzi huo wa marudio.

Baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 Rais Dk. Mwinyi, alikutana pamoja na upinzani uliokuwa unaongozwa na Saif Sharrif Hamad (sasa ni marehemu) akiwa Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo.

Aidha, katika uchaguzi huo alikuwa mgombea mwenzake wa kiti cha urais wa Zanzibar katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

Pande mbili hizo kutoka CCM na ACT- Wazalendo zikakubaliana kuzika tofauti za kisiasa na uhasama na hatimaye kurejesha tena maridhiano ya kisiasa na kuendelea na SUK.

Serikali hiyo ambayo kwa sasa Dk. Mwinyi anaiongoza akiwa na wasaidizi wengine ndani ya Baraza la Mawaziri lenye wajumbe kutoka CCM na ACT-Wazalendo, linaendelea kuifikisha Zanzibar kwenye bandari ya upendo, umoja na usalama.

**AMANI NA UTULIVU**

Mafanikio ya mwaka mmoja ya uongozi wa Rais Hussein Mwinyi yanabebwa na kuimarika kwa amani na utulivu visiwani hapa.

Sasa upo utulivu ambao ni matunda ya kazi ya SUK iliyowaunganisha wananchi wote na kuzika tofauti za kisiasa.

Uamuzi wa kuwapo kwa maridhiano hayo ya kisiasa uliwavutia watu wengi wakiwamo wananchi wa kawaida pamoja na mabalozi wanaowakilisha mataifa mbalimbali waliopo nchini.

Juhudi hizo zinaonekana kuwa ni hatua ambayo imesaidia kumaliza siasa za chuki na uhasama wa kisiasa.

''Nimefurahishwa na maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa kati ya vyama viwili vya kisiasa ambayo lengo lake kubwa kumaliza siasa za chuki na uhasama na kufungua ukurasa mpya wa maelewano,'' anasema Balozi wa Marekani nchini.

Balozi Donald Wright, anayasema hayo wakati akizungumza na Dk. Mwinyi Ikulu visiwani Zanzibar hivi karibuni.

Mwanadiplomasia huyo wa Marekani anaeleza jinsi alivyoridhishwa na juhudi hizo zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Nane katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa lengo la kuimarisha ustawi wa wananchi.

Balozi Wright anamhakikishia Rais Mwinyi kwamba Serikali ya Marekani iko tayari kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza sekta mbalimbali za kimaendeleo.

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa –UNDP, linasimama na Rais Mwinyi, likisema limeridhishwa na kuwapo kwa mazingira ya amani na utulivu Zanzibar baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu na kuundwa SUK.

Mkurugenzi Mkazi wa UNDP, aliyeko Zanzibar Karna Soro, anasema mazingira ya kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa yamesaidia kumaliza mivutano ya kisiasa ambayo ilikuwa ikiathiri maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

"Kwa upande wetu UNDP tumefurahishwa sana na juhudi zilizochukuliwa na viongozi wa Zanzibar za kumaliza mivutano ya kisiasa wenyewe. Mazingira hayo sasa yamemaliza kabisa malumbano ya kisiasa," anasema.

Aidha, anaongeza kuwa viongozi wa Afrika wanayo nafasi kubwa ya kuleta amani na kulifanya bara hilo kuwa sehemu nzuri ya wananchi wake kuishi kwa amani na utulivu na upendano, kama watafanya kazi ya kumaliza malumbano ya kisiasa na migogoro.

Soro anakumbusha kuwa migogoro iliyodumu Afrika kwa kiasi kikubwa imedumaza maendeleo na kulirudisha nyuma bara hilo katika sekta mbalimbali za uchumi,elimu jamii na maendeleo.

"Zanzibar inayo nafasi ya kuimarisha uchumi kutokana na kuwepo kwa fursa nyingi ikiwamo maendeleo ya sekta ya utalii."

**KUUNGANISHA WAZANZIBARI**

Vyama vya siasa Zanzibar wameridhishwa na uongozi wa Rais Dk. Mwinyi Mwenyekiti wa Chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatib, anasema Rais Mwinyi amekidhi matarajio ya wapigakura waliomchagua kwa kuwaunganisha katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo imefuta na kuondosha siasa za chuki na uhasama.

Anasema kuwapo kwa amani ya kudumu kumefungua fursa kwa wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na kutafuta maisha kwa amani na utulivu, hatua ambayo pia imewavutia wawekezaji kuwekeza katika miradi mbalimbali ya uwekezaji na uchumi.

''Maridhiano ya kisiasa yamefungua milango ya amani na utulivu wa kisiasa kitendo ambacho kimemwinua Rais Mwinyi na kuwa kipenzi cha Wazanzibari wote kwa kuwaunganisha. Ndiyo maana tunaona leo hii hata wawekezaji wamejitokeza kwa kasi kuwekeza, kwenye visiwa vyetu,'' anasema.

Naibu Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Nassor Ahmed Mazrui, ambaye chama chake kinaunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa, anasema SUK imewaunganisha Wazanzibari na kumpongeza Rais.

Anasema hatua iliyowezesha kupata uongozi wa pamoja ni kuendeleza misingi ya amani, utulivu na umoja miongoni mwa Wazanzibari.

**PEMBA SHWARI**

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Samala Mbarouk Kharib, anasema wananchi wa mkoa huo wameondokana na siasa za chuki na uhasama ambao awali ziliota mizizi katika mkoa huo.

Anasema hali ya amani na utulivu katika mkoa huo inazidi kuimarika kutokana na uwepo wa SUK.

Anasema maendeleo yaliyofikiwa katika mkoa huo yanatokana na ushirikiano mkubwa uliopo kati ya Serikali ya Mkoa, CCM pamoja na vyama vyengine vya siasa ikiwamo ACT-Wazalendo.

SUK ni matokeo ya uamuzi wa wananchi wa Zanzibar ambao walipiga kura na kutaka iwepo kwa ajili ya kumaliza chuki za kisiasa.

# Undani wa ufanisi wake kuelekea kileleni miaka 60 Uhuru wa nchi

**Na Mwandishi Wetu**



Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MAKTABA.**

NI siku nyingi zimepita, miongo na karne zimebadilika tangu siku ya Uhuru hadi mahali iliko sasa kuelekea umri miaka 60, kileleni siku 35 zijazo.

Mvua ya chama kimoja hadi mvua za demokrasia ya vyama vingi, tumekutana na masika za utawala bora na neema ya kujenga nchi.

Tangu awamu ya kwanza ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius, Nyerere, Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete, John Magufuli na sasa wa awamu ya Samia Suluhu Hassan.

Awamu zote zimegawanyika katika namna ya uendeshaji nchi, mamlaka na utendaji wake, hata kutofautiana kifikra, pamoja na mtazamo wa kuijenga Tanzania.

Sitaki kuwa mwalimu wa awamu zilizopita, bali nisimame katika awamu ya sita tuliyopo leo na tunayoendelea kuishi nayo sasa.

Hata hivyo, asili ni jambo muhimu na hawezi kuikataa abadani, ila mifumo ya jambo lolote jipya linaegemea kwa kuchota asili zetu zilizopita. Mwalimu Nyerere, alikuwa na falsafa ya Kujisahihisha. Ni Wakati wa Kujisahihisha na historia mpya!

Tangu alipoingia madarakani mapema Machi mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, amesimama aking'arisha historia mpya katika siasa za Afrika Mashariki.

Kwa vipi? Mosi ni mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya urais katika ukanda uliopo wa Afrika Mashariki na vizazi vingi vina jambo la kujifunza. Somo kubwa ni la usawa wa kijinsia Tanzania inakuwa imelifikia.

Pia, kuna uhuru wa kuheshimu katiba ya nchi, ambayo ni sehemu ya historia kubwa ambayo inaandikwa ndani ya Tanzania, kwani Rais Samia ameingia madarakani kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Pombe Magufuli, aliyefariki dunia Machi 7, 2021.

Ni wazi fursa iliyopo haitoshi kupambanua Rais Samia Suluhu Hassan, hata hivyo lake nalo lina upekee unaopaswa kutajwa kwa nuru ya pekee.

Kwa Rais Samia iko wazi, mbali na kuiva kiitikadi, pia amekomaa katika falsafa ya uliberali wa jamii na uchumi, ambayo anaamini ni wajibu wa serikali kuinua hali za maisha ya wananchi kwa kuwapatia uhuru wa kuendeleza shughuli zao, bila ya kuingiliwa na serikali.

**MAKUSANYO JUU**

Pia, ndani ya hilo kuna mtazamo wa serikali kurekebisha uchumi au kuratibu uhuru wa biashara na ushindani katika soko, hali inayojidhihirisha baada ya kuleta nafuu ya tozo za kisheria kwenye baadhi ya bidhaa, ili kuwasaidia wananchi.

Baadhi ya taasisi zilizoguswa na maelekezo hayo ya kiserikali ni: Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (tozo ya udhibiti); Mamlaka ya Bandari (tozo ya miundombinu); na Mamlaka ya Mapato Tanzania (tozo ya kuchakata taarifa).

Rais Samia amechukua hatua hiyo kukabiliana na upandaji bei mafuta katika soko la dunia, hali ambayo imekuwa ikiwaathiri watumiaji nchini.

Moja ya maeneo, ni pale namna Rais Samia anavyoonyesha uumini wa ongezeko la kodi linaloendana, sambamba na ukuaji vipato vya wananchi vitokanavyo na shughuli halali za uchumi wa wananchi.

Ili mara tu baada ya kuingia madarakani, Rais Samia alinukuliwa akisema hatopenda kuwapo ukusanyaji kodi kwa namna ya mabavuu. Ni mantiki iliyojidhihirisha kunifanikisha kukusanya Sh. trilioni 5.151.

Hiyo kimsingi, ni asilimia 94 ya lengo la ukusanyaji Sh. trilioni 5.462, kiasi ambacho hakijawahi kufikiwa kwenye kipindi kama hicho miaka mitano iliyopita, tena pasipo kutumia mabavu.

Ni jambo lililoibua pongezi kutoka pande nyingi, kwani inajenga ishara ya mwanzo mzuri unaowachochea watu wengi kulipa kodi kwa hiari, hata kujengea udhihirisho wa staili ya Rais Samia, kwamba ni kiongozi anayesimamia sheria, haki, kanuni na taratibu bila ya woga. wala ubaguzi.

> Mkuu huyo wa nchi, hata kabla ya hapo ameishi ndani ya mfumo wa Muungano na hata ameweza kuzifanyia kazi haraka zaidi na kuziambia mamlaka husika kuchukua hatua kufikia hatua chanya.

**WASIFU ZIADA**

Kuna sifa kubwa anayopatiwa Rais Samia, kwamba mtu anayefuatilia jambo mpaka matokeo chanya yapatikana. Kwa kipindi cha miezi sita ya madaraka, ameshatatua kero 11 za Muungano.

Mkuu huyo wa nchi, hata kabla ya hapo ameishi ndani ya mfumo wa Muungano na hata ameweza kuzifanyia kazi haraka zaidi na kuziambia mamlaka husika kuchukua hatua kufikia hatua chanya.

Hata hivyo, kuna asilopepesa nalo macho, yu mkali hasa dhidi ya kinachoitwa 'fedha za umma', kwa kuahidi kuonyesha alichokitaja "rangi yake kamili kiutendaji ".

Jambo muhimu linalotajwa katika anayosinamia kwa umakini ni kuwapo ubadhirifu kazini, hata ikashukia kwa mtihani mkubwa kwa safu ya Baraza la Mawaziri, ambao ndio 'askari wa mwamvuli' wa kusimamia fedha za umma zilete matokeo.

**MPITO WA KAULIMBIU**

Itakumbubwa muasisi wa Taifa, Mwalimu Nyerere alikuwa na usemi wa namna nyingi katika miaka 24 ya uongozi wake. Wakati katika harakati za Uhuru na siku za mwanzo baada ya Uhuru wa Tangayika, aliuhamasisha umma kwa kaulimbiu "Uhuru ni kazi ya TANU."

Baadaye akadumu na "Uhuru na Kazi" huku mwaka 1964, kabla ya kuchukua uamuzi mzito kitaifa katika mikakati mbalimbali ya maendeleo, aliwekea kolezo "inawezekana, timiza wajibu wako."

Ulipofika uongozi awamu ya pili mwaka 1985, Rais Ali Hassan Mwinyi aling'aa na falsafa ya "Ruksa" huku mrithi wake, Benjamin Mkapa, mwaka 1995 akaibuka na "mtaji wa masikini ni nguvu zake mwenyewe" akiigani na falsafa ya "ukweli na uwazi."

Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, kaulimbiu aliyoingia nayo madarakani mwaka 2005, ilikuwa "Maisha Bora kwa Kila Mtanzania" na Awamu ya Tano ya, John Pombe Magufuli "Hapa kazi Tu", kabla ya mrithi wake aliyeko madarakani akisimamia usukani "Nawasalimu kwa jina la Jamhuri?...kazi iendelee!"




Rais Dk. Hussein Mwinyi alipoihutubia Zanzibar, amefikisha mwaka mmoja sasa katika uongozi wake. **PICHA: MTANDAO**

# Mwaka mmoja Rais Mwinyi Z'bar

## Yajaa manukato ya maridhiano, upatanisho, Pemba sasa ni raha

**Na Rahma Suleiman,**

**ZANZIBAR**

JANA Novemba 2, Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametimiza mwaka mmoja tangu alipoapishwa kuiongoza Zanzibar baada ya uchaguzi mkuu wa 2020.

Siku 365 Ikulu kwa Dk. Mwinyi zina mengi ya kujivunia ambayo yamepatikana ndani ya mwaka mmoja ya uongozi wake.

Ajenda kubwa ya mafanikio yake iko kwenye kuleta maridhiano ya kisiasa visiwani Zanzibar ambapo miaka ya nyuma kabla ya uongozi wake maridhiano hayo yalitetereka.

Kwa nyakati tofauti katika kipindi cha harakati za kampeni za kisiasa mwaka 2020, Dk. Mwinyi, anasisitiza kuwa hafurahishwi na mivutano ya kisiasa iliyopo visiwani humo wakati huo ambao athari zake ni kubwa kijamii na kiuchumi.

'Nikichaguliwa kuwa rais wa Zanzibar nitarudisha amani na utulivu uliopo na kuondoa siasa za chuki na uhasama ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikirudisha nyuma maendeleo ya kijamii na uchumi. Zimesababisha migogoro na chuki," ananukuliwa akisema Dk. Mwinyi.

Anayasema hayo kipindi hicho akigombea urais kwa tiketi ya CCM.

Hawakukosea wahenga waliosema kuwa ahadi ni deni hivyo kutokana na msimamo wa kuwa mpatanisho msemo huo wa wahenga, ulitimia Rais Mwinyi baada ya kupata ridhaa ya kuiongoza Zanzibar alilipa deni kwa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) na kusaidia kuondoa na kupunguza mihemko ya kisiasa.

Ingawa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilikuwapo kabla ya uongozi wa Dk. Mwinyi, ilitetereka baada ya kufutwa kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 na kufanyika tena uchaguzi wa marudio mwaka 2016 ambapo chama kikuu cha upinzani kwa wakati huo CUF hakikushiriki.

Hapo ndipo SUK ilipoanza kutetereka na Zanzibar kuendelea kuongozwa na chama kimoja pekee cha CCM ambacho kilishinda kwa asilimia 99 katika uchaguzi huo wa marudio.

Baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 Rais Dk. Mwinyi, alikutana pamoja na upinzani uliokuwa unaongozwa na Saif Sharrif Hamad (sasa ni marehemu) akiwa Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo.

Aidha, katika uchaguzi huo alikuwa mgombea mwenzake wa kiti cha urais wa Zanzibar katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

Pande mbili hizo kutoka CCM na ACT- Wazalendo zikakubaliana kuzika tofauti za kisiasa na uhasama na hatimaye kurejesha tena maridhiano ya kisiasa na kuendelea na SUK.

Serikali hiyo ambayo kwa sasa Dk. Mwinyi anaiongoza akiwa na wasaidizi wengine ndani ya Baraza la Mawaziri lenye wajumbe kutoka CCM na ACT-Wazalendo, linaendelea kuifikisha Zanzibar kwenye bandari ya upendo, umoja na usalama.

**AMANI NA UTULIVU**

Mafanikio ya mwaka mmoja ya uongozi wa Rais Hussein Mwinyi yanabebwa na kuimarika kwa amani na utulivu visiwani hapa.

Sasa upo utulivu ambao ni matunda ya kazi ya SUK iliyowaunganisha wananchi wote na kuzika tofauti za kisiasa.

Uamuzi wa kuwapo kwa maridhiano hayo ya kisiasa uliwavutia watu wengi wakiwamo wananchi wa kawaida pamoja na mabalozi wanaowakilisha mataifa mbalimbali waliopo nchini.

Juhudi hizo zinaonekana kuwa ni hatua ambayo imesaidia kumaliza siasa za chuki na uhasama wa kisiasa.

''Nimefurahishwa na maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa kati ya vyama viwili vya kisiasa ambayo lengo lake kubwa kumaliza siasa za chuki na uhasama na kufungua ukurasa mpya wa maelewano,'' anasema Balozi wa Marekani nchini.

Balozi Donald Wright, anayasema hayo wakati akizungumza na Dk. Mwinyi Ikulu visiwani Zanzibar hivi karibuni.

Mwanadiplomasia huyo wa Marekani anaeleza jinsi alivyoridhishwa na juhudi hizo zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Nane katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa lengo la kuimarisha ustawi wa wananchi.

Balozi Wright anamhakikishia Rais Mwinyi kwamba Serikali ya Marekani iko tayari kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuendeleza sekta mbalimbali za kimaendeleo.

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa –UNDP, linasimama na Rais Mwinyi, likisema limeridhishwa na kuwapo kwa mazingira ya amani na utulivu Zanzibar baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu na kuundwa SUK.

Mkurugenzi Mkazi wa UNDP, aliyeko Zanzibar Karna Soro, anasema mazingira ya kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa yamesaidia kumaliza mivutano ya kisiasa ambayo ilikuwa ikiathiri maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

"Kwa upande wetu UNDP tumefurahishwa sana na juhudi zilizochukuliwa na viongozi wa Zanzibar za kumaliza mivutano ya kisiasa wenyewe. Mazingira hayo sasa yamemaliza kabisa malumbano ya kisiasa," anasema.

Aidha, anaongeza kuwa viongozi wa Afrika wanayo nafasi kubwa ya kuleta amani na kulifanya bara hilo kuwa sehemu nzuri ya wananchi wake kuishi kwa amani na utulivu na upendano, kama watafanya kazi ya kumaliza malumbano ya kisiasa na migogoro.

Soro anakumbusha kuwa migogoro iliyodumu Afrika kwa kiasi kikubwa imedumaza maendeleo na kulirudisha nyuma bara hilo katika sekta mbalimbali za uchumi,elimu jamii na maendeleo.

"Zanzibar inayo nafasi ya kuimarisha uchumi kutokana na kuwepo kwa fursa nyingi ikiwamo maendeleo ya sekta ya utalii."

**KUUNGANISHA WAZANZIBARI**

Vyama vya siasa Zanzibar wameridhishwa na uongozi wa Rais Dk. Mwinyi Mwenyekiti wa Chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatib, anasema Rais Mwinyi amekidhi matarajio ya wapigakura waliomchagua kwa kuwaunganisha katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo imefuta na kuondosha siasa za chuki na uhasama.

Anasema kuwapo kwa amani ya kudumu kumefungua fursa kwa wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na kutafuta maisha kwa amani na utulivu, hatua ambayo pia imewavutia wawekezaji kuwekeza katika miradi mbalimbali ya uwekezaji na uchumi.

''Maridhiano ya kisiasa yamefungua milango ya amani na utulivu wa kisiasa kitendo ambacho kimemwinua Rais Mwinyi na kuwa kipenzi cha Wazanzibari wote kwa kuwaunganisha. Ndiyo maana tunaona leo hii hata wawekezaji wamejitokeza kwa kasi kuwekeza, kwenye visiwa vyetu,'' anasema.

Naibu Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Nassor Ahmed Mazrui, ambaye chama chake kinaunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa, anasema SUK imewaunganisha Wazanzibari na kumpongeza Rais.

Anasema hatua iliyowezesha kupata uongozi wa pamoja ni kuendeleza misingi ya amani, utulivu na umoja miongoni mwa Wazanzibari.

**PEMBA SHWARI**

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Samala Mbarouk Kharib, anasema wananchi wa mkoa huo wameondokana na siasa za chuki na uhasama ambao awali ziliota mizizi katika mkoa huo.

Anasema hali ya amani na utulivu katika mkoa huo inazidi kuimarika kutokana na uwepo wa SUK.

Anasema maendeleo yaliyofikiwa katika mkoa huo yanatokana na ushirikiano mkubwa uliopo kati ya Serikali ya Mkoa, CCM pamoja na vyama vyengine vya siasa ikiwamo ACT-Wazalendo.

SUK ni matokeo ya uamuzi wa wananchi wa Zanzibar ambao walipiga kura na kutaka iwepo kwa ajili ya kumaliza chuki za kisiasa.





## Wanafunzi 120,000 wapatiwa mafunzo usalama barabarani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ZAIDI ya wanafunzi 120,000 kwenye mikoa mbalimbali nchini wamepata mafunzo ya usalama barabarani ili kujiepusha na ajali.

Mafunzo hayo yametolewa katika mikoa ya Dar es Salaam, Geita, Ruvuma, Dodoma, Mwanza, Kilimanjaro na Zanzibar na Puma Energy Tanzania Ltd kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la AMEND.

Ofisa Uhusiano wa kampuni hiyo, Godluck Shirima, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Puma, Dominic Dhanah, aliyasema hayo jana kwenye hafla ya kutoa zawadi kwa wanafunzi wa shule za msingi zilizoshinda shindano l a michoro ya usalama barabarani kwa mwaka 2020/21, jijini hapa.

Alisema utoaji wa zawadi hizo unahitimisha mradi uliotekelezwa na Puma na Amend ambao ulihusisha mafunzo kuhusu usalama barabarani na uchoraji wa picha kwa shule za Kisasa, Ipagala B, Chidachi, Makole na Dodoma Mlimani ambapo wanafunzi wasiopungua 20,000 walipata mafunzo hayo.

"Huu mpango wa usalama barabarani ni mwendelezo wa kampeni ambayo ilizinduliwa rasmi miaka tisa iliyopita ambapo zaidi ya shule 100 zimefikiwa na wanafunzi zaidi ya 120,000 mikoa mbalimbali wamepata mafunzo hayo," alisema.

Alisema kwa njia hiyo Puma Energy inaamini kuwa watoto watakuwa salama na kutakuwa na taifa lenye watu imara na wenye nguvu za kulitumikia taifa lao.

"Lengo letu kama kampuni ni kuongeza wigo ili kufikia shule nyingi zaidi nchi nzima kwa mwaka 2022, sisi kampuni ya Puma Energy tunaahidi kuendelea kuwekeza katika kampeni ya usalama barabarani kwa kushirikiana na serikali kupitia Jeshi la Polisi ili kuokoa maisha ya Watanzania," alisema.

# Waandishi 23 wafanyiwa ukatili wakati wakitimiza majukumu yao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Habari Tanzania (MCT) limesema katika kipindi cha miezi 10, waandishi wa habari 23 kutoka vyombo mbalimbali wamekumbwa na mikasa wakati wakitimiza majukumu yao.

Pamoja na kukumbwa na mikasa kama vile kupigwa, kunyang'anywa vifaa vya kazi, kunyimwa taarifa, kukamatwa, kutishwa na kufungiwa kwa vyombo vyao, matukio hayo yamepungua ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita.

Ofisa Programu Mwandamizi wa MCT, Paul Mallimbo, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa tamko la kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kukomesha Ukatili dhidi ya Wanahabari kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Kajubi Mukajanga.

Alisema waandishi hao walikumbwa na mikasa hiyo kuanzia Januari hadi Oktoba, mwaka huu ikiwamo vyombo vitatu kufungiwa, mwandishi mmoja aliuawa, waandishi tisa walikamatwa ama kwa maagizo ya wakuu wa wilaya wakiwataka kwenda kuandika maelezo yao au kukamatwa baada ya kuchapisha au kurusha habari.

"Matukio mengine yaliyojitokeza katika kipindi cha miezi 10 iliyopita ni kwa waandishi watatu kunyimwa taarifa katika taasisi za umma, kupigwa na kudhalilishwa lilikuwa moja, vitisho matukio matatu, kuharibiwa vifaa na kuondolewa katika eneo la kufanyia kazi kwa nguvu tukio moja," alisema.

"Matukio haya yamepungua ikilinganishwa na kipindi cha mwaka 2018 hadi 2019. Kanzidata ya MCT ilirekodi matukio 119 ya ukiukwaji wa haki za waandishi wa habari, kipindi hiki kilikuwa na matukio mengi ya magazeti kufungiwa na vituo vya runinga kutozwa faini," aliongeza.

Malimbo alisema kwa mwaka 2020 matukio yalikuwa 41 na idadi kubwa ilikuwa katika kipengele cha waandishi wa habari kukamatwa na kati ya hayo vyombo vya habari 13 vilitozwa faini na vinne kufungiwa.

"Hali ya kutojali au ya watenda maovu kutowajibishwa kwa matendo yao, ambayo husababisha tabia hiyo kukomaa kwa kuwa waovu hawana hofu tena ya kuchukuliwa hatua yoyote ndiyo huitwa 'impunity'," alisema.

Katika kuadhimisha hayo, Malimbo alizikumbusha mamlaka kuwa kumekuwapo na matukio mabaya yaliyowakuta wanahabari ambayo hayajachunguzwa na kufikia hatima ikiwamo la kupotea kwa mwandishi Azory Gwanda.

Pia alisema kumekuwa na matukio kadhaa ya vyombo vya habari kushinda kesi mahakamani, lakini mamlaka zinapuuzia uamuzi wa mahakama jambo linalochafua taswira ya taifa.

Aliwahimiza wanahabari kuendelea kuripoti matukio yote ya ukiukwaji wa haki za waandishi yanayowakuta lakini pia kufanya kazi zao kwa kuzingatia weledi na maadili ya taaluma.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma, Dk. Evance Chande (kushoto), akipewa maelezo na Chifu Lazalo Chihoma (katikati), alipotembelea kwenye himaya yake ya makumbusho yaliyoko Bwibwi, Kata ya Iyumbu, kuona na kujifunza zana mbalimbali zilizokuwa zikitumiwa na machifu kikiwamo kinu kilichotengenezwa mwaka 700, kilichokuwa kikitumika kwa kazi ya kukoboa nafaka na kutwangia dawa za kienyeji. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Gwajima: Tunathamini mchango wa AZAKI

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema serikali inathamini mchango wa asasi za kiraia nchini na itaendelea kuzitambua kwa kazi nzuri zinazofanya kwa ajili ya manufaa ya taifa.

Dk. Gwajima aliyasema hayo juzi alipokuwa akitoa tuzo mbalimbali kwa baadhi ya asasi za kiraia zilizofanya vizuri zaidi katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma baada ya kumalizika kwa Wiki ya AZAKI.

Alisema asasi zote zinafanya vizuri lakini tuzo hizo zimetolewa kwa wale walioonyesha ubunifu na kujitolea zaidi katika utendaji kazi zao katika kuhakikisha wananchi wanafaidika na miradi wanayoiendesha katika mashirika yao.

"Tunapoikuza jamii yetu ya Kitanzania tunamsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kutekeleza maono yake kwenye taifa hili. Nipende kumshukuru kwa maono yake amekuwa akihamasisha tuzidi kuimarisha ushirikiano na asasi za kiraia," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, alipongeza AZAKI kwa midahalo iliyofanyika inayolenga kuimarisha utekelezaji, kuboresha majukumu hayo.

"Nyie kama wadau wa maendeleo mkaonyeshe kweli kuwa nyie ni wadau kwa kulenga kuleta matokeo zaidi na kubuni namna ya kupata rasilimali kwa ajili ya kuendeleza shughuli zenu," alisema.

Alisema wizara itaendelea kutoa ushirikiano kwa asasi zote za kiraia ikiwamo utoaji wa miongozo mbalimbali na kuwahimiza waendelee kufanya kazi kwa bidii kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni zilizopo.

Naye Rais wa Asasi za Kiraia, Dk. Stigmata Tenga, aliishukuru serikali kwa kuthamini mchango wa AZAKI na kuwapa nafasi katika kuchangia maendeleo ya Taifa kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa na asasi hizo kwenye maeneo tofauti nchini.

"Wizara imekua ikionyesha kutusikiliza na kukaribisha mawazo yetu hivyo kututia moyo zaidi kuendelea kufanya kazi," alisema.



# TAKUKURU yaonya matumizi fedha za corona

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, imewatahadharisha watumishi wote watakaohusika na utafunaji wa fedha za corona ambazo zimetolewa na serikali kwa ajili ya kufanya shughuli za maendeleo katika sekta za afya, elimu na barabara.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Denis Manumbu, alitoa onyo hilo jana wakati akizungumza na wanahabari ofisini kwake juu ya utekelezaji wa shughuli za taasisi hiyo kwa kipindi cha robo ya mwaka kuanzia Julai, mwaka huu.

Alisema tayari serikali imeingiza fedha za corona kwenye halmashauri zote za mkoa wa Mbeya na kuwaomba watumishi wote watakaopewa nafasi ya kusimamia miradi kuwa waaminifu kujiepusha na vitendo vya rushwa.

"Nawatahadharisha watumishi wote wa umma fedha za UVIKO- 19 (corona) zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa kila halmashauri imepewa fedha, tunaendelea kufuatilia na kufanya uchunguzi kwa yeyote atakayebainika atachukuliwa hatua za kisheria," alisema Manumbu.

Pia Manumbu alisema taasisi hiyo imefanikiwa kukagua miradi yenye thamani ya Sh. bilioni tano na taarifa 124 zilikaguliwa na kubainika na tuhuma za rushwa na makosa mengine.

Alibainisha kuwa kati ya hizo, taarifa 56 zilihusu rushwa na 68 hazikuhusu rushwa baadhi ya kesi hizo uchunguzi umekamilika na nyingine unaendelea.

Katika taarifa yake, Manumbu alizinyooshea kidole taasisi binafsi na halmashauri kuwa kinara wa vitendo vya rushwa na kwamba Halmashauri ya Jiji la Mbeya katika kitengo cha manunuzi inaongoza kwa vitendo vya rushwa.

Aliongeza kuwa TAKUKURU imewapa elimu wananchi 23,749 kupitia semina mbalimbali zilizoandaliwa ili kutokomeza vitendo vya rushwa mkoani Mbeya.

Hivi karibuni, mkoa wa Mbeya ulipokea Sh. bilioni 15 kwa ajili ya mapambano dhidi ya corona ambao umeisumbua dunia.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema fedha hizo zinagawiwa kwa halmashauri kulingana na mahitaji ya kuboresha miundombinu ya afya, elimu, barabara na maji.

Aliwaomba viongozi kusimamia fedha hizo kwa uaminifu ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.




Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU), mkoa wa Mbeya, Denis Manumbu, akizungumza na waandishi wa habari, mkoani humo jana, kuhusu utekelezaji wa robo ya mwaka katika mapambano ya vitendo vya rushwa. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# DC ahamasisha jamii bima ya afya

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

MKUU wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, amewahamasisha wananchi kujiunga na Bima ya Afya iliyoboreshwa (iCHIF) ili kuwa na uhakika wa matibabu kwa gharamu nafuu.

Dk. Anney alitoa rai hiyo juzi wakati akizungumza na Nipashe juu ya mwamko wa wananchi kujiunga na mfuko huyo katika Wilaya ya Rungwe.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo wana uchumi mzuri ambao wanaweza wakautumia kuchangia mfuko huo wa Bima ya Afya kwa Sh. 30,000 kwa mwaka mzima kiwango ambacho aidai kitawasaidia wao na familia zao kutibiwa.

"Jiungeni na bima inasaidia sana kwenye matibabu. Magonjwa huwa hayapigi hodi kwa hiyo huwezi ukajua kwamba utaugua lini. Unaweza kuugua siku ambayo huna hela lakini ukiwa na bima unatibiwa bila matatizo," alisema Dk. Anney.

Katika hatua nyingine, Dk. Anney alisema serikali inaendelea kuboresha hospitali ya wilaya na kwamba serikali imetoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya ukarabati wa baadhi ya majengo yaliyochakaa.

Vilevile aliweka jiwe la msingi kwenye jengo la mama na mtoto katika hospitali hiyo ambalo limejengwa kwa gharama ya Sh. milioni 481 na lina vyumba 42.

# Wachimbaji wa madini walia ubovu barabara

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

MWENYEKITI wa Wachimbaji Madini Mkoa wa Mbeya, Salum Manyesha, ameiomba serikali kuboresha miundombinu ya barabara kuelekea maeneo ya shughuli za uchimbaji madini ili kuwarahishia usafirishaji wa bidhaa hiyo sokoni.

Manyesha alisema hayo juzi wakati akizungumza na wanahabari wanawake kutoka maeneo mbalimbali nchini ambao walifanya ziara wilayani hapa kuangalia shughuli za uchimbaji madini.

Alisema Wilaya ya Chunya imebarikiwa kuwa na madini karibu kila eneo na kwamba wananchi wanategemea shughuli hiyo kuendesha maisha yao hiyo kuboreshwa miundombinu ya barabara na huduma nyingine kutarahisha shughuli hiyo.

"Tunaomba wanahabari mtufikishie kilio chetu kwa serikali bado kuna tatizo ya miundombinu kwenye maeneo ya machimbo na maeneo mengine hayafikiki kabisa kwa kuwa sekta ya madini inachangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa tunaomba tukumbukwe ili tufanye shughuli zetu kwa uhuru," alisema Manyesha.

Aidha, aliipongeza serikali kwa jitahada zake za kufungua soko kubwa la madini ambalo linahudumia wachimbaji wote wa madini wilayani Chunya kwa madai kuwa soko hilo limewapunguzia gharama za usafiri kwenda maeneo ya mbali kuuza bidhaa hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, alisema sekta ya madini ndiyo inategemea kufanikisha shughuli zote za maeneo katika eneo hilo na kwamba inaendelea kuboresha huduma muhimu katika maeneo ya migodi ili kuwawezesha wachimbaji kutimiza majukumu yao na kujiongezea kipato.

**"Tunaomba wanahabari mtufikishie kilio chetu kwa serikali bado kuna tatizo ya miundombinu kwenye maeneo ya machimbo na maeneo mengine hayafikiki kabisa kwa kuwa sekta ya madini inachangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa tunaomba tukumbukwe ili tufanye shughuli zetu kwa uhuru," alisema Manyesha.**

# SMZ kujenga shule ya wenye uhitaji maalum

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema ifikapo mwaka 2022 inatarajia kujenga shule ya watoto wenye mahitaji maalum Unguja na Pemba ili watoto waweze kupata elimu kama wengine.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Juma Khamis, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema kwa Unguja shule hiyo itakuwa Jendele katika eneo lenye hekari 15 na kisiwani Pemba ni Chakechake ambako tayari kuna hekari 13.

Alisema shule hizo zitakuwa na bweni kwa watoto wote wenye mahitaji maalum katika mahitaji yao.

Katibu huyo alieleza kuwa ujenzi huo pia utahusisha, maeneo ya michezo, maduka, kilimo na ufugaji kwa lengo la kumwangalia uwezo wa mtoto na kumwelekeza panapomfaa kwa ajili ya kujifunza.

Aidha, alisema serikali itahakikisha inaweka mazingira mazuri yatakayoweza kumwandaa mtoto huyo ili kuona kila mmoja anasoma na kujifunza.

Naye Katibu wa Jumuiya ya Watoto wanaoishi na vichwa vikubwa na mgongo wazi Zanzibar, Hussein Mohammed Saleh, alisema suala la kupata elimu kwa watoto wenye tatizo la mgongo wazi na vichwa maji ni changamoto kubwa kwa sababu wanakosa miundombinu ya kuweza kufikia shule.

Alisema wingi wa watoto hao wanaishi na vifaa vinavyoitwa mpira (shanti) na inakuwa hatarishi kwa kuchanganyika na jamii nyingine.

"Kwa kuliona hili wazazi pia wana wasiwasi wa kuwapeleka watoto wao katika shule za kawaida kuchanganyika na watoto wenzao kwa kuhofia usalama wao," alisema.

**Naye Katibu wa Jumuiya ya Watoto wanaoishi na vichwa vikubwa na mgongo wazi Zanzibar, Hussein Mohammed Saleh, alisema suala la kupata elimu kwa watoto wenye tatizo la mgongo wazi na vichwa maji ni changamoto kubwa kwa sababu wanakosa miundombinu ya kuweza kufikia shule.**

# Rais Mwinyi amwahidi ushirikiano kiongozi UNICEF

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amempongeza Kiongozi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) ofisi za Zanzibar, Laxm Bhawani, kwa kazi kubwa na nzuri inayofanywa na ofisi hiyo na kumhakikishia kuwa serikali itaendelea kumuunga mkono ili kufikia mafanikio katika maeneo anayofanyia kazi.

Dk. Mwinyi alisema hayo juzi Ikulu Zanzibar, wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na mwakilishi wa huyo.

Alisema ofisi hiyo inafanya kazi kubwa kuhakikisha huduma mbalimbali ikiwamo za afya na elimu zinaimarika nchini, kuondokana na umaskini na utapia mlo kwa watoto.

Alisema upatikanaji wa lishe kwa watoto ni jambo muhimu na kubainisha kazi kubwa inayopaswa kufanyika kufanikisha jambo hilo kwa kuzingatia takwimu zilizopo za watoto wenye utapia mlo.

Alisema katika kuimarisha huduma za afya, serikali imekuwa ikifanya juhudi kubwa uwekaji wa miundombinu katika sekta hiyo pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wake.

Dk. Mwinyi, alitoa mfano wa dhamira ya serikali ya kujenga hospitali katika wilaya zote Unguja na Pemba na kuwapo mahitaji makubwa ya wafanyakazi wa huduma za afya katika nyanja mbalimbali. Rais Dk. Mwinyi alisema serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imefanya juhudi kuona kwa namna gani itaweza kuimarisha kiwango cha elimu nchini kupitia sera ya elimu iliyopo.

Kiongozi wa UNICEF, Bhawani kwa upande wake, alimweleza Rais Dk. Mwinyi masuala mbalimbali yanayotekelezwa na ofisi yake ikiwamo ya kufanikisha programu ya ulimwengu ya kuwarejesha watoto shule, mitaala ya walimu ya kuinua viwango vya ufundishaji na hatua ya kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwamo mradi wa kunusuru kaya maskini (TASAF) katika kufanikisha mpango wa kupunguza umaskini nchini.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika (BOA) Tanzania, Adam Mihayo (kulia), akipata maelezo ya mchakato wa kuhifadhi samaki kwa Mkurugenzi wa kampuni ya kuuza samaki nje ya nchi ya Zan Oceanic International, Suleiman Seif, alipokuwa kwenye ziara ya kutembelea wateja wakubwa wa benki hiyo, kisiwani Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMWA yapongeza wanawake kwa uteuzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Wahabari Wanawake Tanzania (TAMWA Zanzibar), kimewapongeza wanawake walioteuliwa hivi karibuni kuiongoza Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kisiwani humo.

Wanawake hao ni Salma Ali Hassan Khamis ambaye ni Mkurugenzi wa Mashtaka na Mwanamkaa Abdulrahman Mohammed, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Tunguu, Mkurugenzi wa TAMWA, Dk. Mzuri Issa, alisema, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar ina majukumu mengi yakiwamo ya kupokea na kukagua majalada yote yanayotoka polisi, kuchambua ushahidi wa upelelezi uliotoka polisi, kupeleka majalada ya kesi mahakamani, kuendesha kesi mahakamani kwa kuuwakilisha upande wa serikali na kukata rufani iwapo haitaridhika na uamuzi wa mahakama kuhusiana na shauri lolote.

Alipongeza uteuzi huo uliofanywa na Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi kwa kuwaamini wanawake na kuwapa nafasi mbalimbali za uongozi.

"Hawa ni viongozi wa kwanza wanawake kuongoza ofisi hiyo katika nafasi hizo kuu kabisa na hivyo kuongeza uwapo wa wanawake katika nafasi za uongozi kwa jumla, hali ambayo inahimizwa kwa maendeleo ya mwanamke na nchi kwa jumla," alisema Dk. Mzuri.

Alisema TAMWA inaamini kuwa kuwapo kwa viongozi hao, kesi za udhalilishaji na ukatili wa wanawake na watoto zitapata msukumo mpya katika ufuatiliaji na uchunguzi na kwa muda mfupi ili kukomesha kabisa vitendo hivyo vilivyokithiri nchini.

Dk. Mzuri aliwashauri wateule hao kuandaa utaratibu maalum wa kushirikiana na Jeshi la Polisi ili kurahisisha uchunguzi katika matukio ya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, jumla ya kesi 838 za udhalilishaji ziliripotiwa kuanzia mwezi wa Januari hadi Agosti, 2021, wanawake walioathirika ni 679 sawa na asilimia 81 na wanaume ni 166 sawa na asilimia 19.8.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

GARI INAUZWA AINA YA VOLKSWAGEN TOUREG YA MWAKA 2004 NAMBA DDV RANGI NYEUSI. INATEMBEA NA IKO KWENYE HALI NZURI SANA. BEI NI TSH. 15,000,000/- PIGA SIMU NAMBA 0762 810 451.

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



17 16548702

**ALLAN CHARLES ZACHARIA** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0342-0074** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **SHAABAN ROBERT** mwaka 2010, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **KW/RB/5275/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



116548802

**CAMILA JAMES KASULWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1619/0014** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia VICTORY SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/512934/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MIRATHI NAMBA:187/2019**

**MUOMBAJI......................SOPHIA RAMADHAN MBARAKA**

**DHIDI YA**

**MDAIWA:....................................MAHAMUDU ATHUMAN**

**OMBI LA ..........................SOPHIA RAMADHAN MBARAKA**

**MADAI YA..................UTEKELEZAJI SHAURI LA MIRATHI**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 19 mwezi 11 mwaka 2021 saa 2:00 Asubuhi.
Angalia kama *hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakam ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 22 mwezi 10 mwaka 2021

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO.

116549102

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ROSEMARY S MAAJAR anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye namba za usajili T 566 DHD chasisi namba ACA21-0116622 engine namba IAZ4005888,y-eyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa CONTROL NAMBA 9910830265284

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa wa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi Na 96, 2021**

**Katika shauri la mirathi ya ZUBERI LIHEMULA MSHELE.....Marehemu wa Ramadhani.**

**Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa na CHARLES ZUBERI MSHELE...... Mwombaji.**

**TANGAZO KWA UMMA.**
(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi mahakama ya mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuudhuria katika shauri hili nendapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe...17....... mwezi ...11..... mwaka ...2021.....kabla ya huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo,mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.
Zingatia ;Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe ...1.... mwezi ...11.... Mwaka...2021.....

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIAGORETH JOSEPH AUGUSTINO** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 395 DPK – SUZUKI KEI.** Chassis namba **HN225831586.** Engine namba **K6A4098948.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/SEL/RB/523276/2021.**

116549802

## KUFUNGA KAMPUNI

**THE GIFT ARENA LIMITED (124051).**
PLOT No. 499/101, JAMAA STREET, ILALA. P.O. BOX 7822 DAR ES SALAAM.
PRIVATE COMPANY ANATANGAZA KUFUNGA KAMPUNI KUANZIA LEO **3/11/2021.**

116550202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 161/2021**

**MDAI: SALIMU MUSWANDIKO HASSANI**

**DHIDI YA**

**MDAIWA 1. NASRA HAJI**
**2. KHARIFA OMURO**
**WA**
**POPOTE WALIPO TANZANIA BARA NA VISIWANI**

**AMRI:**
Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 03/11/2021 Saa 2:30 Asubuhi bila kukosa. Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo,na kutolewa uamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo Jumatano 20 tarehe 10 mwezi 2021

HAKIMU
PRIMARY COURT MAGISTRATE GEITA

116550302

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**SUMMONS FOR ORDERS**
**(Rule 8 subodinate Courts(Civil Procedure Summons and Pleadings)**
**(Rules,1955)**

**In the District court of.........Mbeya..............At.................**
**Civil Case No....59.................of 2001.................Highland ........seed...... Growers.................................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**BONIFACE......M......MGAYA ....................DEFENDANT**
**To: BONIFACE......M......MGAYA..........................**

**WHEREAS** the above named Plaintiff(s)has/have instituted a suit against you upon the claim, particulars which are set out in the copy of the plaint with annexure attached hereto; **YOU ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within twenty one (21) days of the service of this summons upon you.if there are more than one Plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed suffiecient on each of the plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence,there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.
**AND TAKE NOTICE** that if you default in filing of the written statement of defence within the time specified, the court may pronounce judgment against you.
Given under my hand the Seal of the Court This 26 day of October,2021.

**DISTRICT/RESDENT MAGISTRATE**
**Mention on 09/11/2021**




Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Samia ataja athari mabadiliko tabianchi kwa Tanzania

Na Christina Mwakangale

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema pamoja Tanzania kuwa na hifadhi ya misitu ya takribani hekta milioni 48, inashuhudia athari za mabadiliko ya tabianchi kama kwenye nchi zingine duniani na kwamba zinahitajika juhudi za haraka kwa nchi zilizoendelea kuziwezesha zinazoendelea kiuchumi kukabili hali hiyo.

Amesema athari hizo zimesababisha ongezeko la kina cha maji baharini, joto huku Mlima wa Kilimanjaro ukipoteza mwonekano wake wa asili na barafu kwenye kilele, kuyeyuka.

Rais Samia aliyasema hayo jana wakati akihutubia kwenye Mkutano wa 26 wa Umoja wa Mataifa (COP 26) unaojadili athari za mabadiliko ya tabianchi, jijini Glasgow, nchini Scotland.

"Tanzania hatujaachwa kando na kinachotokea katika athari hizi, tunashuhudia kina cha bahari kuongezeka na ardhi kumezwa, fahari yetu ya Mlima Kilimanjaro barafu kwa kiasi kikubwa inayeyuka, tunashuhudia mafuriko na ukame visivyotabirika," alisema Rais Samia.

Alibainisha kwamba visiwani Zanzibar kunashuhudiwa viwango vya juu vya joto, kuliko ilivyozoeleka na kusababisha kuharibu mfumo wa ikolojia katika sekta ya utalii.

"Kwa nchi maskini kama Tanzania, inamaanisha asilimia 30 ya Pato la Taifa (GDP), linalotokana na kilimo, misitu na uvuvi, haliwezi kuwa endelevu, kunahitaji hatua zaidi kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ingawa kasi ni ndogo licha ya mkataba wa Paris ili kufikia 1.5 nyuzi joto malengo," alisema Rais Samia.

Alisema inachukua hatua kadhaa ili kukabiliana na mabadiliko hayo na baadhi kuhatarisha mipango ya taifa na ajenda katika maendeleo, ikihitajika kuanzishwa 'green house' 30 hadi 35 ikiwa ni mkakati wa kukuza uchumi hadi ifikapo 2030.

"Tunaongeza kasi ya upandaji miti ila mwaka huu mkakati ni kupanda miti milioni 276. Nchi zinazoendelea tumeonyesha hatua hizi kwa nini zilizoendelea zijiweke kando. IPCC imeeleza athari za mabadiliko ya tabianchi, tunafahamu kinachohitajika na nchi kama yetu itaathirika.

"Tunaita uwezeshaji wa haraka katika hili ili kukabiliana na vyanzo vya mabadiliko ya tabianchi wakati wa mabadiliko ni sasa."

Akizungumza juzi katika mjadala wa wazi wa viongozi kwenye mkutano wa 26 wa nchi wanachama wa mkataba wa mabadiliko ya tabianchi, CO26, Rais Samia alisema mshikamano na juhudi za viongozi katika kukabili mabadiliko ya tabianchi vitapimwa si kwa ahadi kubwa wanazotoa mkutanoni, bali kwa jinsi wanavyotekeleza vipengele vyote vya mkataba wa Paris wa mabadiliko ya tabianchi.

Alivitaja vipengele hivyo kuwa ni pamoja na kupunguza makali ya mabadiliko ya tabianchi, kuhimili mabadiliko hayo sambamba na uchangiaji wa fedha kulingana na kiwango cha changamoto zilizoko hivi sasa.

"Mabadiliko ya tabianchi ni suala la dunia nzima na hivyo majawabu yake ni lazima yawe ya kimataifa na hivyo tunatoa wito kwa nchi zilizoendelea ambazo ndiyo zinaongoza kwa uchafuzi zitekeleze kwa vitendo ahadi zao za kupunguza madhara kwa kutoa fedha za kutosha kufanikisha malengo yetu kwenye michango ya kitaifa ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa uendelevu."

Alisisitiza fedha za misaada ya fedha itakuwa ni msingi katika mikakati yetu ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kwamba Tanzania na nchi zingine za kipato cha chini zimeandaa mpango wa NDC's ikiwa na mikakati dhahiri ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

"Mipango yetu ni mtambuka katika sekta zote muhimu, lakini hatuwezi kufanikisha bila usaidizi wa kutosha na teknolojia inayotakiwa ili kujenga uwezo wetu.

> "Tunahitaji kuufanya mkutano huu wa COP26 kuwa ni wakati ambao tunauelewa ukweli kuhusu mabadiliko ya tabianchi.



Rais Samia Suluhu Hassan (katikati) akiwa pamoja na Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson (kushoto), na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, baada ya kuwasili ukumbi wa mikutano jijini Glasgow, nchini Scotland, juzi, 2021. **PICHA: TOVUTI YA RAIS**

### KATIBU MKUU UN

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres, awali alituma ujumbe mzito kwa dunia akisema, dunia inachimba kaburi lake yenyewe.

"Tunachimba makaburi yetu wenyewe. Macho na masikio ya dunia sasa yako Glasgow, Scotland, katika mkutano wa viongozi wa dunia. Inatosha kuharibu bayoanuwai, kuiua hewa ukaa, kutumia maliasili kama choo, kuchoma, kuchimba na kujitumbukiza katika shimo zaidi."

Guterres alisema, sayari ya dunia inabadilika mbele ya macho ya watu, kuanzia kwenye barafu inayoyeyuka, hadi hali mbaya ya hewa isiyoisha.

"Tunakabiliwa na chaguo la ama tuyazuie au yatuzuie. Masuala matano ni muhimu kwa viongozi wa dunia. Kina cha bahari sasa ni mara mbili ya kiwango cha miaka 30 iliyopita, bahari imekuwa na joto zaidi kuliko hapo awali, sehemu za msitu wa mvua wa Amazon sasa hutoa hewa ya kaboni zaidi kuliko unavyofyonza.

"Matangazo ya hivi majuzi ya hatua za mabadiliko ya tabianchi yanaweza kutoa hisia kwamba tuko njiani kugeuza mambo. Huu ni udanganyifu, hata kama ahadi za hivi majuzi zilikuwa bayana na za kuaminika na kuna maswali mazito juu ya baadhi hizo bado tunajali janga la mabadiliko ya tabianchi."

Aidha, wanaharakati wa mabadiliko ya tabianchi wako mstari wa mbele kutaka sauti zao zisikike katika mkutano huo.

"Tunataka wakuu wa nchi wawe viongozi wa kweli na wawe chachu ya mabadiliko na kuchukua hatua wakati wa COP26", alisema Juan Pablo Sierra, mwanaharakati kijana kutoka Shirika lisilo la kiserikali NGO la United for Climate Action.

Wanaharakati wawili vijana walifuatia kupanda jukwaani, wakitoa wito kwa viongozi kuchukua hatua za ujasiri.

"Nyinyi nyote mna uwezo wa kuwa bora zaidi, kukumbuka kwamba kwa maneno yenu mna silaha zinazoweza kutuokoa au kutuuza. Hauhitaji maumivu yangu au machozi yangu kumaliza shida hii. Sisi si tu waathirika wa mgogoro huu, sisi ni mawakala wa matumaini. Hatuzami, tunapambana," walisema wanaharakati hao.

Boris Johnson, Waziri Mkuu wa Uingereza, awali alisema changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ni kiama.

"Tunahitaji kuufanya mkutano huu wa COP26 kuwa ni wakati ambao tunauelewa ukweli kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Tunaweza kupata hali halisi," alisema Boris.

HABARI MICHEZO

# REDONDO AAHIDI MAKUBWA AKITOA SIRI KUITWA STARS

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI mpya aliyechaguliwa kwenye kikosi cha timu ya soka ya Tanzania, Taifa Stars, Ramadhani Chombo 'Redondo', ameeleza furaha yake ya kuitwa kwenye kikosi hicho na kuahidi kuitumikia kwa mapenzi na moyo wake wote kama Mtanzania, huku akifunguka siri ya kucheza kwa muda mrefu kwa kiwango kikubwa.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Redondo alisema kitendo cha kuitwa kwake timu ya taifa, kimezidi kumfanya afikirie kujituma zaidi kwani anaona wapo watu wanaofuatilia wachezaji wanaofanya vizuri kwenye michezo mbalimbali ya Ligi Kuu na mingine.

"Kusema kweli nimefurahi sana. Mimi ni Mtanzania, najivunia kuchaguliwa kuitetea nchi yangu na naahidi nitaitumikia kwa moyo wangu wote nikishirikiana na wenzangu. Pia imenipa ari ya kujituma zaidi kwa sababu inaonyesha kuwa kumbe kuna watu wanathamini na wanaona wachezaji wanaojituma na kufanya vizuri kwenye mechi mbalimbali," alisema mchezaji huyo ambaye amewahi kuzitumikia klabu za Ashanti, Simba na Azam FC.

Mchezaji huyo mkongwe alisema siri ya yeye kuendelea kucheza kwa kiwango cha hali ya juu na kuwazidi hata vijana, ni kujitunza, kujituma kwenye mazoezi, lakini pia kutokuwa majeruhi mara kwa mara na majereha sugu ambayo husababisha kiwango cha mchezaji kushuka.

Mchezaji huyo ni mmoja kati ya wachezaji 27 walioitwa na kocha Kim Poulsen, kwenda kujiandaa na mechi mbili za kuwania kufuzu Kombe la Dunia Qatar 2022 dhidi ya DR Congo na Madagascar, hiyo ikiwa ni mara ya kwanza kwake kujumuishwa katika kikosi hicho tangu mwaka 2015.

Kiungo huyo mshambuliaji aliichezea Simba mwaka 2010, baadaye 2012 alijiunga na Azam, kabla ya kurejea Simba 2014.

**UZINDUZI...**



Waimbaji wa Kikundi cha Friends of Jesus cha Kanisa la Waadventista Wasabato Mbezi Luis, Dar es Salaam wakiingia kanisani mwishoni mwa wiki kwa wimbo maalum kwa ajili ya uzinduzi wa albamu zao tatu ziitwazo 'Ni Mwema, Shangwe na Jina la Yesu'. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Kampuni ya Mdundo yaweka rekodi Afrika*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI bora ya huduma za muziki mtandaoni ya Mdundo Records, imeweka rekodi ya kipekee barani Afrika baada ya kufikisha idadi ya watumiaji milioni 16.4 kwa kipindi cha robo tatu cha mwaka wa 2021, kilichoishia Septemba, mwaka huu.

Matokeo hayo ni ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa ni robo iliyotangulia, ambapo ongezeko hilo limechangiwa na idadi kubwa ya watumiaji wapya kutoka nchi za Tanzania, Kenya na Afrika Kusini.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, Tanzania iliongoza kwa kuwa na watumiaji wapya 4.1 walioripotiwa, huku Nigeria na Kenya zikirekodi watumiaji wapya milioni 3.1 na milioni 2.6.

Nchini Tanzania, kampuni ya Mdundo Records ilikua kwa asilimia 36 kutokana na watumiaji wapya milioni 4.1, hivyo kuchangia asilimia 24 ya jukwaa la watumiaji wa kampuni hiyo katika kipindi hicho cha robo tatu ya mwaka wa 2021.

Akizungumzia mafanikio hayo, Mkuu wa Mdundo Brand Partnerships Africa, Rachel Karanu, alisema huo ni ushahidi tosha kuwa taasisi yao ni kichocheo dhabiti katika kukuza biashara kwa kuvutia wateja zaidi kupitia kitengo chao cha matangazo cha Mdundo For Brands.

"Tunafanya kazi kwa karibu sana na chapa zinazoongoza kibiashara barani Afrika, hivyo mafanikio haya ni habari njema kutokana na ukweli kwamba chapa ya Mdundo na wateja wetu inawafikia wateja wengi sana barani kote.

"Tunatarajia kukuza wigo wa jukwaa letu kwa kuwafikia wateja wengi zaidi katika robo ya mwisho ya mwaka 2021, hivyo kuongeza thamani za bidhaa za wateja wetu," alisema.

Kwa mujibu wa uongozi wa taasisi hiyo, kampuni hiyo inafanya kazi na baadhi chapa bora za kibiashara katika nchi za Kenya, Nigeria na Tanzania.

Katika kipindi cha robo tatu cha mwaka, kampuni hiyo imeweza kushughulikia ukuaji wa chapa wa makampuni bora barani Afrika ambayo ni pamoja na SportPesa, Safaricom, Chrome Gin, Standard Chartered Bank, Captain Morgan, Coca Cola, BetKing na Guinness Smooth kwa kutaja machache.

Miradi ya chapa imejikita kwenye vifaa vipya vya kuboresha chapa iliyozinduliwa hivi karibuni ya Mdundo Brand Lift Tool na ambayo inapatikana bila malipo kupitia tovuti ya mdundoforbrands.com, ambapo inatoa bila malipo taarifa muhimu kuhusiana na wateja na chapa zao.

Kupitia Mdundo Brand Lift Tool, Mdundo imefanikiwa kufanya tathmini ya utendaji kazi kwa wakati huku ikitoa taarifa ya mafanikio ya kampeni zake kwa wateja wake zinazohusiana na mafanikio ya chapa zao yanayotokana na uhamasishaji kupitia matangazo mbalimbali.

## Kocha Polisi aivulia kofia Mbeya Kwanza

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, ameipongeza Mbeya Kwanza kwa kuweza kurudisha mabao yote mawili ndani ya dakika tano tu, kipindi cha pili dhidi ya timu yake, pia akimsifia kocha wa timu hiyo, Haruna Hererimana kwa mbinu zake bora.

Malale aliimwagia sifa Mbeya Kwanza, baada ya timu yake kulazimishwa sare ya mabao 2-2 juzi kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, wakati timu yake ikiwa inaongoza mabao 2-0 hadi mapumziko.

"Niwapongeze wapinzani wetu. Wamepambana na kurudisha mabao yote mawili, si jambo rahisi kufungwa mabao mawili na kurudisha yote. Nimpongeze pia kocha wa timu ya Mbeya Kwanza kwa mbinu zake kwa sababu kabla wachezaji wangu hawajajua cha kufanya, tayari walikuwa wamerudisha mabao yote na waliposhtuka, wapinzani wetu walikuwa wameshajipanga kuzuia," alisema Malale.

Naye kocha Hererimana, pamoja na kujipongeza kwa sare hiyo, lakini alisema wachezaji wake wana tabia ya kujisahau kipindi cha kwanza.

## Uhamiaji sasa hasira kwa Black Sailor leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa Timu ya Uhamiaji, Khamis Aman "Gulity" amesema matokeo ya sare ya bao 1-1 waliyoyapata dhidi ya Taifa Jang'ombe katika mechi yao wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar haikuwa mipango yake.

Gulity aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea mchezo wake wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Black Sailor utakaopigwa leo.

Alisema kupata matokeo ya sare katika mchezo wa kwanza hayakuwa matokeo mazuri katika mechi ya kwanza ya ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Alisema kukosa umakini kwa wachezaji ndicho kitu kilichowakosesha matokeo katika mchezo huo, lakini amefanyia kazi kasoro hizo kuelekea mchezo wao wa leo.

"Tumecheza vizuri na wachezaji wamejitahidi kutokana na ugumu wa mechi yenyewe, hivyo makosa madogo madogo ni kitu cha kawaida katika soka na tayari nimefanyia kazi," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CONTE RASMI SPURS

ANTONIO Conte anajiandaa kutia saini mkataba wa pauni milioni 20 kama kocha mpya wa Tottenham Hotspur. ***(Telegraph)***

### NEWCASTLE KUTANGAZA KOCHA

KLABU ya Newcastle United inapanga kumtangaza kocha wao mpya wiki hii, huku kocha wa zamani wa Villarreal, Unai Emery, 49, akitajwa kuwa na nafasi kubwa. ***(Mirror)***

### VILLA WAMTAKA FONCECA

ASTON Villa wamefanya mawasiliano yasiyo rasmi na kocha wa zamani wa AS Roma, Paulo Fonseca wakati klabu hiyo ikimfikiria kujaza nafasi ya Dean Smith. ***(Mail)***

### BARCA KUMFUATA XAVI

KLABU ya Al Sadd imewaambia maofisa wa Barcelona kwenda nchini Qatar kuridhia makubaliano kwa ajili ya Xavi, 41. ***(AS)***

### CONTE ATAKA FUNGU

ANTONIO Conte amemuomba Mwenyekiti wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy fungu la bajeti la karibu pauni milioni 237 kwa ajili ya kuwanunua wachezaji kutoka Serie A aliowabainisha. ***(Calciomercato, via Express)***

### XAVI AMTAKA POGBA

XAVI ameipatia Barcelona orodha ya wachezaji wanne anaotaka kuwasajili, akiwamo kiungo wa kati wa Manchester United, Paul Pogba, 28, ambaye mkataba wake utamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(El Nacional)***

### NUNO KUJAZWA NOTI

KLABU ya Tottenham Hotspur inajiandaa kumlipa, Nuno Espirito Santo kitita cha pauni milioni 14, lakini kipengele cha mkataba wa kocha huyo raia wa Ureno kingeruhusu Spurs kumfukuza bila malipo mwishoni mwa msimu huu kama angeshindwa kumaliza kwenye sita bora katika Ligi Kuu ya England. ***(Sun)***

### ASENSIO AGOMBEWA

LIVERPOOL na Arsenal ni miongoni mwa klabu tano zilizotoa ofa ya kumsajili, Marco Asensio, 25, kutoka Real Madrid Januari, sambamba na Juventus, AC Milan na Borussia Dortmund. ***(El Nacional)***

### IBRAHIMOVIC MKATABA MPYA

AC Milan inajiandaa kutoa ofa kwa mshambuliaji wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic , 40, ofa hii ni ongezeko la mkataba mpya kwa makubaliano yaleyale ya mkataba wa sasa. ***(Calciomercato)***

### ARSENAL YAMTAKA BELOTTI

ARSENAL wanafikiria uhamisho wa mshambuliaji wa Torino, Andrea Belotti, 27, raia wa Italia. ***(Calciomercato)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AGUERO NJE YA DIMBA BARCA MIEZI MITATU

●●● Mchezaji wa kikosi cha kwanza, Sergio amefanyiwa uchunguzi na anaendelea na...

**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Sergio Aguero, atakuwa nje ya uwanja kwa muda wa miezi mitatu wakati akiendelea kufanyiwa matibabu ya moyo na mishipa ya damu.

Aguero alitolewa nje wakati wa mchezo wa sare ya bao 1-1 wa LaLiga dhidi ya Deportivo Alaves mwishoni mwa wiki baada ya kupatwa na kizunguzungu na kujisikia maumivu ya kifua.

Nyota huyo wa zamani wa Manchester City alikimbizwa hospitali kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa moyo na hatakuwa kwenye kikosi cha Barca hadi angalau Februari 2022.

**Taarifa ya klabu hiyo ilithibitisha: "Mchezaji wa kikosi cha kwanza, Sergio Aguero amefanyiwa uchunguzi na anaendelea na matibabu chini ya daktari, Josep Brugada.**

"Hatakuwapo kwenye kikosi cha timu kwa kipindi cha miezi mitatu ijayo hadi atakapokuwa fiti baada ya matibau kwa ajili ya kuangalia hali yake."

Aguero ameanza kwenye mechi mbili tu tangu ajiunge na Barca baada ya kumaliza kipindi chake cha miaka 10 kucheza kwenye Ligi Kuu England.

Miamba hao wa Catalunya leo Jumanne watacheza na Dynamo Kiev kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wa Kundi E, ambapo wapo nafasi ya tatu baada ya mechi tatu.

MECHI KALI

HOME AWAY

SIMBA

1.22 | 5.41 | 10.63

NAMUNGO

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 642



# HAZARD HATAKI KUONDOKA REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

NYOTA wa Real Madrid, Eden Hazard, hana mpango wa kuondoka kwenye Jiji la Madrid katika dirisha la usajili la Januari, kwani bado anahitaji kupambania nafasi yake kwenye kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Carlo Ancelotti.

Hazard ambaye ana wakati mgumu tangu asajiliwe akitokea Chelsea mwaka 2019 kwa ada ya kitita cha euro milioni 100, amecheza michezo 39 kwenye Ligi Kuu ya Hispania LaLiga kwa zaidi ya miaka miwili sasa.

Hazard kwa msimu ulioisha amekosa michezo 33 kutokana na kuwa majeruhi, huku kukiwa na uvumi kwamba Madrid wanampango wa kumuacha ili kupunguza hasara kwa sababu ya mejeraha ya mara kwa mara.

Kocha Ancelotti ameweka wazi kuwa chaguo lake la kwanza ni Rodrygo na Hazard atakuwa kwenye foleni kumsubiri.

Lakini Hazard mwenyewe amethibisha kuwa anabaki na yupo tayari kupigania namba na hana mpango na dirisha la usajiri la Januari.

"Januari? Sina mpango wa kuondoka Madrid kwa sasa, kwa sababu bado ninamkataba wa kuendelea kucheza hapa," alisema Hazard akinukuliwa na gazeti la Marca.



# *Solskjaer: Nafurahia sana kukosolewa*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema anafurahia sana kukosolewa na hana nia ya kupambana na yeyote anayemkosoa.

Solskjaer Jumamosi aliiongoza Man United kwenye ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Tottenham Hotspur wikendi iliyopita, lakini bado alikosolewa kwa mbinu mbovu alizotumia.

Ushindi huo dhidi ya Spurs umempunguzia presha ingawa bado ana kibarua cha kuwavaa Atalanta leo Jumanne nchini Italia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pia Solskjaer na kikosi chake wanaisubiria Manchester City kwenye Ligi Kuu England, wikendi hii.

"Kukosolewa kunaweza kukufanya ukawa na wasiwasi au unaweza kusimama imara," alisema Solskjaer akinukuliwa na Sky Sport kuelekea mchezo wa leo Jumanne wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta.

"Mara zote nimekuwa nikifurahia kukosolewa, acha wanikosoe, sina shaka, waandishi, wachambuzi na magwiji, sote tuna kazi zinazotofautiana, ni kazi yao kutoa maoni sipo hapa kwa ajili ya kupambana nao."



## HABARI MICHEZO


# 2,668,240 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/11/21 | 18:00 | Crystal Palace vs Wolverhampton | 2.42 | 3.14 | 3.04 |
| 02. 06/11/21 | 18:00 | Blackburn vs Sheffield Utd | 2.32 | 3.29 | 2.89 |
| 03. 06/11/21 | 18:00 | Luton Town vs Stoke City | 2.27 | 3.21 | 3.06 |
| 04. 06/11/21 | 18:00 | Barnsley vs Hull City | 2.44 | 3.09 | 2.89 |
| 05. 06/11/21 | 20:30 | Alaves vs Levante | 2.55 | 3.05 | 2.95 |
| 06. 06/11/21 | 20:30 | Blackpool vs QPR | 2.44 | 3.28 | 2.74 |
| 07. 07/11/21 | 17:00 | Everton vs Tottenham | 2.65 | 3.15 | 2.75 |
| 08. 07/11/21 | 17:00 | Nantes vs Strasbourg | 2.38 | 3.23 | 2.98 |
| 09. 07/11/21 | 17:00 | Leeds vs Leicester | 2.85 | 3.45 | 2.39 |
| 10. 07/11/21 | 17:00 | Udinese vs Sassuolo | 2.47 | 3.44 | 2.75 |
| 11. 07/11/21 | 20:30 | Osasuna vs Real Sociedad | 2.94 | 3.24 | 2.43 |
| 12. 07/11/21 | 22:45 | Rennes vs Lyon | 2.89 | 3.48 | 2.32 |
| 13. 07/11/21 | 23:00 | Betis vs Sevilla FC | 2.80 | 3.21 | 2.55 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 03 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 08:00 | 3651 | FC Tokyo vs Shimizu S Pulse | 1.95 | 3.38 | 3.43 |
| 08:00 | 5794 | Yokohama vs Sagan Tosu | 3.08 | 3.03 | 2.24 |
| 09:00 | 1405 | Nagoya Grampus vs Kashiwa Reysol | 1.85 | 3.27 | 3.95 |
| 09:00 | 2242 | Sanfrecce Hiroshima vs Kashima Antlers | 2.71 | 3.34 | 2.32 |
| 10:00 | 4175 | Vissel Kobe vs Vegalta Sendai | 1.45 | 4.22 | 5.76 |
| 13:30 | 1018 | Police FC Rwanda vs Espoir FC | 1.70 | 3.50 | 4.42 |
| 14:00 | 1558 | Coastal Union vs Tanzania Prisons | 1.91 | 2.85 | 4.44 |
| 16:00 | 2380 | Rutsiro FC vs Rayon Sports FC | 2.26 | 2.99 | 3.09 |
| 16:00 | 2821 | Biashara United vs Mbeya City | 2.11 | 2.84 | 3.66 |
| 16:00 | 3987 | APR FC vs Musanze | 1.21 | 5.61 | 10.63 |
| 16:00 | 5934 | Gicumbi vs Etoile de Lest | 2.30 | 3.14 | 2.89 |
| 16:30 | 2696 | Amazulu vs Tshakhuma | 1.99 | 3.09 | 3.93 |
| 16:30 | 3624 | Catanzaro vs Palermo | 2.03 | 3.18 | 3.42 |
| 16:55 | 1216 | Al Wehda vs Al Khaleej Club | 2.54 | 3.36 | 2.45 |
| 17:00 | 1042 | Baniyas vs Emirates Club | 1.36 | 5.00 | 6.15 |
| 17:00 | 2557 | Modena vs Piacenza Calcio | 1.56 | 3.75 | 5.20 |
| 17:00 | 5018 | AL Urooba vs AL Khaleej Khor Fakkan | 2.74 | 3.85 | 2.11 |
| 17:15 | 5588 | Al Ahli Doha SC vs Al-Shamal | 1.93 | 3.62 | 3.28 |
| 17:15 | 5845 | Al Rayyan SC vs Al Gharafa SC | 2.21 | 3.70 | 2.65 |
| 17:50 | 4797 | Alshoulla vs Al Orubah | 2.14 | 3.18 | 3.14 |
| 18:00 | 1923 | MAS Maghrib A Fes vs Sccm Chabab Mohammedia | 2.11 | 3.03 | 3.37 |
| 18:00 | 3968 | Cape Town City vs Chippa Utd | 2.08 | 3.04 | 3.72 |
| 18:30 | 1192 | Mamelodi Sundowns vs Maritzburg Utd | 1.44 | 4.13 | 7.08 |
| 19:00 | 2173 | Bugesera FC vs Etincelles | 2.23 | 3.12 | 3.02 |
| 19:00 | 4796 | Suduva vs Zalgiris | 2.89 | 3.17 | 2.28 |
| 19:00 | 5091 | Simba vs Namungo | 1.22 | 5.41 | 10.63 |
| 19:45 | 2015 | Al Ahli Jeddah vs AL Baten | 1.76 | 4.07 | 3.92 |
| 19:55 | 5274 | Lekhwiya SC vs Al Sadd SC | 4.25 | 4.35 | 1.58 |
| 20:15 | 4326 | Raja Casablanca vs Rapide Oued Zem | 1.28 | 5.01 | 8.29 |
| 20:45 | 2100 | AC Milan vs Porto | 1.95 | 3.55 | 3.75 |
| 20:45 | 2122 | Real Madrid vs Shakhtar Donetsk | 1.25 | 5.93 | 10.78 |
| 21:00 | 4273 | Amorebieta vs Valladolid | 4.71 | 3.09 | 1.84 |
| 21:00 | 5341 | Mirandes vs Lugo | 2.07 | 3.10 | 3.64 |
| 22:30 | 2208 | Olympique Khouribga vs Wydad Casablanca | 5.21 | 3.57 | 1.59 |
| 22:30 | 2669 | Teramo vs Pescara Calcio | 3.32 | 3.22 | 2.05 |
| 22:30 | 5636 | Foggia vs Fidelis Andria | 1.53 | 3.75 | 5.58 |
| 22:45 | 1286 | Barnsley vs Derby | 2.21 | 3.13 | 3.23 |
| 22:45 | 1813 | Cardiff vs QPR | 2.61 | 3.25 | 2.56 |
| 22:45 | 3998 | Bournemouth vs Preston | 1.57 | 3.91 | 5.28 |
| 22:45 | 4453 | Blackpool vs Stoke City | 2.95 | 3.24 | 2.31 |
| 22:45 | 5968 | Blackburn vs Fulham | 3.53 | 3.58 | 1.93 |
| 23:00 | 1679 | Borussia Dortmund vs Ajax | 2.42 | 3.80 | 2.60 |
| 23:00 | 2580 | Manchester City vs Brugge | 1.14 | 7.76 | 18.55 |
| 23:00 | 2892 | West Bromwich vs Hull City | 1.37 | 4.61 | 7.45 |
| 23:00 | 3147 | Sheriff Tiraspol vs Inter | 9.22 | 5.61 | 1.29 |
| 23:00 | 3453 | Sporting Lisbon vs Besiktas | 1.39 | 4.89 | 7.39 |
| 23:00 | 3559 | RB Leipzig vs Paris St Germain | 2.73 | 3.56 | 2.42 |
| 23:00 | 4656 | Liverpool vs Atletico Madrid | 1.66 | 4.00 | 4.80 |
| 23:15 | 4744 | Eibar vs Real Oviedo | 1.87 | 3.19 | 4.31 |
| 23:15 | 5283 | Las Palmas UD vs Fuenlabrada | 1.73 | 3.25 | 5.12 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# PSG KUVUNJA MKATABA NA RAMOS




**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain inafikiria kuvunja mkataba na beki, Sergio Ramos waliyemsajili miezi michache iliyopita akitokea Real Madrid, kwa mujibu wa Jarida la Les Parisien.

PSG wanaangalia vipengele kadhaa katika mkataba waliompatia beki huyo ili waweze kutafuta njia sahihi wanayoweza kuachana naye, akiwa hajacheza mechi yoyote hadi sasa.

Ramos mwenye umri wa miaka 35, alisajiliwa kama mchezaji huru katika majira ya joto, lakini hajafanikiwa kucheza mchezo wowote akiwa na PSG kutokana na majeraha yanayomuandama hadi sasa.

PSG wanadai hawakupewa taarifa sahihi na za kutosha kuhusu majeraha ya mchezaji huyo wakati wa usajili wake na wako tayari kuvunja mkataba ili wapunguze gharama za mshahara.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, PSG inaweza kuachana na mchezaji huyo wakati wowote kuanza sasa na atakuwa huru kujiunga na timu yoyote.




# Alaba: Madrid kubwa kwa Bayer kwa kila kitu

**MADRID,** Hispania

DAVID Alaba amesema "kila kitu ni kikubwa" pale Real Madrid ikilinganishwa na timu yake ya zamani, Bayern Munich wakati akijifunza kuzoea mazingira ili kuwa na mafanikio anayoyatarajia.

Baada ya miaka 13 ya Alaba kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, Bundesliga, Bayern Munich, aliondoka Mei mwaka huu kutokana na kukataa ofa ya mkataba mpya hapo Allianz Arena na akajiunga na miamba hao wa LaLiga.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Austria, ameanza katika mechi 13 kati ya 14 za Madrid kwenye mashindano yote msimu huu - ni Eder Militao na Thibaut Courtois pekee wameanza mechi nyingi zaidi yake - wakicheza kwa jumla ya dakika 1,170.

Alaba amecheza kwenye nafasi tofauti na alifunga bao la ufunguzi wakati wa mchezo wa El Clasico ambapo Madrid ilishinda 2-1 dhidi ya wapinzani wao Barcelona, Oktoba 24.

Alaba alikuwa mchezaji wa tano katika historia ya Madrid kufunga kwenye mchezo wake wa kwanza wa Clasico karne hii baada ya Ronaldo wa Brazil (2003), Ruud van Nistelrooy (2006), Raphael Varane na Jese Rodriguez (wote mwaka 2013).

Alaba pia ametoa asisti kwa mabao kadhaa, ikiwa na maana kwamba ni Marco Asensio pekee (mara nne), Vinicius Junior (12) na Karim Benzema (19) ambao wamehusika kwenye mabao mengi kuliko yeye.

Na sasa Alaba ambaye amecheza mechi tano bila kuruhusu bao, amezungumzia mazingira yalivyo hapo Madrid.

"Nahisi kitu tofauti kabisa tangu siku ya kwanza," alisema akiliambia gazeti la Kicker.

"Kila kitu hapa ni kikubwa tofauti na kule Bayern Munich na hapa jiji hili lipo vizuri zaidi."

# Michezo

Jumatano Novemba 3, 2021

Nipashe



Aguero nje Barca miezi mitatu

UKURASA 21

KITAELEWEKA TU...



Wachezaji wa Simba, Pascal Wawa, akimiliki mpira dhidi ya Yusuf Mhilu, wakati wa mazoezi ya timu hiyo ambayo leo itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Namungo FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara raundi ya tano. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Redondo aahidi makubwa Stars

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI mpya aliyeitwa kwenye kikosi cha timu ya soka ya Tanzania, Taifa Stars, Ramadhani Chombo 'Redondo', ameeleza furaha yake...




HABARI UK. 20

## PSG sasa kuvunja mkataba na Ramos

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain inafikiria kuvunja mkataba na beki, Sergio Ramos waliyemsajili miezi...



HABARI UK. 23

# Simba, Namungo ushindi tu leo

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Makocha wote wasema hatoki mtu, majeruhi waongezeka Msimbazi, lakini...

BAADA ya matokeo ya sare mbili mfululizo, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, leo watashuka tena Uwanja wa Benjamin Mkapa wakijaribu bahati yao dhidi ya Namungo FC kwenye mechi ya raundi ya tano itakayopigwa majira ya saa 1:00 usiku huku kila timu ikieleza inachokitaka leo ni ushindi tu.

**Simba ambayo mechi iliyopita ilitoka suluhu dhidi ya Coastal Union uwanjani hapo, itashuka kwenye dimba hilo leo ikiendelea kuwakosa wachezaji wake, Chris Mugalu na Pape Sakho, lakini sasa pakiwa na ongezeko la majeruhi baada ya uongozi wa klabu hiyo kueleza Mzamiru Yassin na Sadio Kanoute nao watakosekana kutokana na kuumia kwenye mchezo uliyopita.**

Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Thierry Hitimana, amesema anaamini timu yake itafanya vizuri kwenye mechi ya leo kwa sababu hata mchezo uliopita, walitengeneza nafasi nyingi, lakini kwa bahati mbaya tu walishidwa kuzitumia.

"Tumejiandaa vizuri, tunakumbuka kuwa mechi iliyopita tulitoka sare nyumbani, tukakosa pointi tatu, watu hawakufurahia, inavyoonekana haikuwa siku yetu, unajua siku zote haziko sawa na hiki ni kama kipindi cha mpito baada ya miaka minne ya mafanikio, kitapita tu.

"Kama uliona kwenye mechi dhidi ya Coastal Union, kipindi cha pili baada ya kufanya mabadiliko, timu ilianza kucheza na kushambulia, bahati mbaya tu, mabao yalikataa kuingia, lakini kwenye mechi hii hali inaweza kuwa tofauti," alisema.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Selemani Matola, amekiri kuwa mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu hakuna mechi yoyote ambayo hucheza na timu iyo ikawa rahisi.

"Hakuna mechi yoyote ambayo tunacheza na Namungo ikawa rahisi, lakini tumejiandaa kupata ushindi, tumejipanga kupata matokeo mazuri. Ni kweli tuna tatizo la kufunga mabao na hiyo inatokana na presha waliyonayo wachezaji wetu kwa sasa na muda ni mdogo wa kulishugulikia, ila tunapambana nalo," alisema.

Hitimana alithibitisha kuwa atawakosa Mugalu na Sakho ambao bado hawajawa fiti, huku wakizalisha majeruhi wengine kwenye mechi iliyopita dhidi ya Coastal Union, Mzamiru na Kanoute.

Kwa upande wa Namungo, Kocha Msaidizi, Godfrey Okoko, amesema wataingia uwanjani kwa kushambulia kwa sababu wanazihitaji mno pointi tatu.

"Kama Simba ambavyo wanazitaka na sisi pia tunazitaka, wachezaji wetu wako vizuri, hatuna majeruhi wala kadi nyekundu. Tunachotaka wachezaji wetu waingie, wapambane na kufanya kile ambacho tumewaagiza," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

Simba inaingia dimbani ikiwa kwenye nafasi ya nne kwa pointi nane huku Namungo ikishika nafasi ya 10 kwa pointi tano baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara nne.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >